**DALADALA** Arusha zagoma kutwa nzima kisa bajaji

UKURASA 2



**WAKILI** afungua kesi ya kupinga Jaji Mkuu kubaki ofisini hadi sasa

UKURASA 4


Nipashe TESA
Jumanne Julai 4, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Wanasayansi wachunguza kasoro zinazoutesa mwili wa binadamu
ELIMU
NA JAMES LAUREAN
Waandae warithi, kuendeleza vitega uchumi utakapokufa
•Wafunze kuzitawala fedha, kuthubutu na nidhamu

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Julai 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581361

www.ippmedia.com


www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


MAZUNGUMZO MAALUM

# Tundu Lissu: Dk. Slaa aje, hajafukuzwa

**AFUNGUKA** kinachoendelea kati yake na Mbowe, kinachomkwaza katika maridhiano...*Endelea ukurasa wa 5*



Lissu Dk. Slaa



## Rais Samia awapa siri wana-SADC maisha yapo kwenye kilimo

UKURASA 2



**MGOMO ARUSHA** Baadhi ya wakazi wa Kwa Morombo jijini Arusha wakiwa wamepakiwa kwenye guta jana kutokana na mgomo wa daladala jijini humo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

UKURASA WA 3

## LATRA YABAINI SHIDA MABASI YA KAMPUNI YA NEW FORCE

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imesitisha ratiba za safari za saa tisa na saa 11 alfajiri kwa mabasi 38 ya Kampuni ya New Force.

Mkoani Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, aliwaambia waandishi wa habari kuwa sababu ya kuondolewa...

## Lori laua ndugu wanne, wamo bwana na bibi harusi wakitoka kufunga ndoa

UKURASA 4

**MICHEZO** YANGA, BIG BULLETS KUVAANA MALAWI UK. 24

**KATUNI** UK. 6




Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Spika wa Bunge, Tulia Ackson, baada ya kuwasili jijini Arusha kwa ajili ya kufungua Mkutano Mkuu wa 53 wa Jukwaa la Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC-PF) uliofanyika jijini humo jana. **PICHA: IKULU**

# Samia awapa siri wana-SADC maisha yapo kwenye kilimo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameziagiza nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kutumia mikakati na sera za kuboresha sekta ya kilimo ili kuufanya ukanda wa nchi hizo kuwa mzalishaji na msambazaji mkubwa wa chakula ndani na nje ya Afrika.

Alitoa agizo hilo jana katika mkutano wa 53 wa SADC uliofanyika jijini hapa.

Rais Samia alisema eneo la SADC, lenye watu milioni 380 kati yao milioni 51.3 hawana chakula ambayo ni makadirio ya mwaka 2020/21 ikiwa ni ongezeko la asilimia 25.7 kutoka la mwaka 2019/20.

Samia alisema katika kipindi cha mwaka mmoja pekee kumekuwa na ongezeko la watu wenye uhitaji wa chakula kwa asilimia 25.7 katika eneo la SADC hali ambayo haikubaliki.

"Hali ni mbaya zaidi na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yanaathiri vibaya sekta ya kilimo katika nchi nyingi za kusini, bado tuna jumla ya kilomita za mraba milioni 9.8 5 ambazo zinaweza kukidhi kapu la chakula la kikanda kwa Afrika na kwingineko, ikiwa imetolewa kwa ufanisi na ipasavyo.

"Pia tuna ardhi kubwa kwa ajili ya kilimo, lakini tunapaswa kufanya chochote tunachopaswa kufanya ili kutumia ardhi hii kwa kilimo au uzalishaji wa chakula. Ili tuzibe pengo ambalo Afrika au eneo la SADC inasemekana kuwa na njaa," alisema.

Alisema maeneo hayo endapo yakitumika vizuri yatasaidia kuwa na utaratibu wa kupatikana kwa chakula kwa kila mtu katika ukanda na kufanikisha dhamira ya utekelezaji wa sera na mikakati mbalimbali ambayo imepitishwa mara kwa mara.

"Tunakuja na mipango mingi ya kisera, lakini hatuitekelezi. Kwa hivyo huu ni wakati ambapo sekta inatekeleza sera zetu za uzalishaji wa chakula," alisema na kuongeza:

"Katika ngazi za kikanda na kimataifa ni lazima tujitolee katika utekelezaji wa ajenda ya mwaka 2063, hasa lengo lake namba tano la kilimo cha kisasa, kuongeza tija na uzalishaji, pamoja na malengo namba mbili, au Malengo ya Maendeleo Endelevu ambazo zinanuia kufikia sifuri ya njaa ifikapo mwaka 2033," alisema.

Kadhalika, alisema katika kuhakikisha vijana wa Tanzania wanapata ajira na nchi kuwa na usalama wa chakula cha kutosha serikali imeanzisha programu maalumu iitwayo BBT kwa ajili ya kuajiri vijana 812 kwenye sekta ya kilimo ambao watawezeshwa ardhi na mitaji.

Alisema Tanzanja imefanikiwa kuanzisha Baraza la Ushauri la Kilimo ambalo jukumu lake kubwa ni kumshauri Rais juu ya mbinu bora na za uhakika katika kuharakisha mabadiliko ya sekta ya kilimo nchini.

"Programu hii ni kwa mujibu wa maazimio ya azimio la matokeo ya mwaka 2004 kuhusu kilimo na usalama wa chakula kwa nchi wanachama wa SADC ambalo linataka serikali kutenga angalau aslimia kumi ya bajeti zao kwa taifa kwa ajili ya kilimo," alisema.

Kadhalika, alisema washiriki wa mkutano huo watapata fursa ya kutembelea moja ya kituo cha BBT kilichopo eneo la Tengeru wilayani Arumeru.

Naye Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alisema katika mkutano hio watajadili mada mbalimbali ikiwamo uwekezaji wa kilimo cha kisasa ili kuzisaidia nchi za SADC ziweze kujitosheleza kwa chakula na kutengeneza ajira kwa ajili ya vijana.

Alisema Tanzania imepiga hatua na fedha nyingi na wadau mbalimbali wamewekeza katika sekta ya kilimo ili kuweza kuzalisha chakula cha kutosha kwa ajili ya kulisha nchi za SADC dunia.

Naye Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alitoa mada iliyohusu kilimo cha kisasa kama njia ya kukabiliana na upungufu wa chakula, alisisitiza kila nchi kuzalisha mazao kwa wingi na kuwauzia wengine, kuacha kuwa tegemezi.

Alisema kwa sasa tishio kubwa linazozikabili nchi nyingi za SADC ukiondoa Afrika Kusini ni upatikanaji wa mbegu bora, jambo ambalo linaweza kukwamisha jitihada za kuwa na uhakika wa chakula.

"Tanzania tumejipanga kuwa na hekta za mraba milioni nane za kilimo cha umwagiliaji ifikikapo mwaka 2030 ili kujiwekea uhakika wa kuzalisha chakula kipindi chote cha mwaka," alisema Bashe.

Alisema nchi za Afrika kuna haja ya kujikita katika ubunifu wa kuboresha sekta za kilimo ili kusaidia wananchi, kwamba mwaka 2018 nchi ya Tanzania ilikuwa na kampuni chache za uzalishaji wa mbegu ila kwa sasa idadi imeongezeka.

Bashe alisema: "Huu siyo wakati wa nchi za Afrika kuomba mbegu kwenye kampuni za nje kwa sababu uwezo tunao na wataalamu pia tunao, tupambane wenyewe kupata mahitaji ya wananchi wetu. Afrika tuache kushindana wenyewe kwa wenyewe badala yake tuungane kwa pamoja kusaidiana kuinua sekta zetu za kilimo."

# Daladala Arusha zagoma kutwa nzima kisa bajaji

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANANCHI wa Jiji la Arusha jana walionja kadhia ya shida ya usafiri baada ya madereva daladala kugoma kufanya shughuli zao, wakishinikiza kuondolewa kwa bajaji katika ruti zao.

Kutokana na mgomo huo uliodumu kutwa nzima, kulikuwa na kero kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ambao jana walipaswa kuripoti shuleni baada ya kuwa likizo kwa mwezi mmoja.

Baadhi ya wananchi wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, akiwamo Fetty Michael, walisema mgomo huo umewaathiri kwa kukosa usafiri.

Michael alisema daladala zinalipa mapato ya Sh. 600,000 kwa mwaka, bima Sh. 250,000 na ushuru wa barabarani. Serikali iliahidi kuleta magari aina ya coaster lakini mwisho wa siku imeruhusu bajaji mjini.

"Je, ni sahihi kuingiza bajaji mjini badala ya kuleta coaster? Ukiangalia bajaji wamechukua mizunguko muhimu ya barabara zilizokuwa za daladala ikiwamo Ngusero, Sanawari, Lemara, Sombetini na Majengo," alisema.

Alibainisha kuwa bajaji zinatakiwa kupaki pembezoni mwa mji na siyo kuingia mjini kwa kuwa huo ndiyo utaratibu lakini haufuatwi.

"Kama bajaji ni chombo cha usafiri wa umma, mbona hawabebi wanafunzi kwa Sh. 200 kama ilivyo kwa daladala kulingana na sheria za LATRA?" alihoji.

Mwananchi mwingine, Mariamu Hamisi, mkazi wa Usa River, alisema alitumia usafiri wa mabasi makubwa yanayokwenda mikoani kwenda katika shughuli zake za kibiashara jana.

"Hali ya usafiri ni shida kwa wafanyabiashara, watumishi wa serikali na wanafunzi kwa kuwa shule zimefunguliwa leo (jana)," alisema Mariamu.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kaloleni, Hamisa Juma, mkazi wa Kata ya Murieti, alisema alikaa katika kituo cha daladala tangu saa 11:57 asubuhi lakini alikosa usafiri.

"Mimi sielewi wanagoma nini na kusababisha wanafunzi tushindwe kwenda shuleni, ukiangalia bajaji hazina msaada kwetu kwa kuwa ni gharama kupanda," alisema.

Mmoja wa madereva daladala, Alfred Kisela, alisema wameweka mgomo wa kubeba abiria kwa kuwa wameingiliwa na bajaji na manyanyaso yamekuwa mengi.

Alisema stendi walizokuwa wanaegesha magari yao zimechukuliwa ikiwamo stendi ndogo ya Kilombero ambayo sasa inatumika kama soko na maegesho ya magari madogo.

Vilevile, dereva huyo alidai kuwa vituo vyao vya kuegesha na kushusha abiria wamekuwa wakigombania abiria na madereva bajaji ilhali hawako katika mzunguko wa katikati ya mji.

"Daladala zinalipa ushuru wa Sh. 700 kila siku na ukitoka stendi unapigwa tochi na watu wa maegesho ya magari, bila kujua hivyo tunajikuta tunadaiwa ushuru ambao hatuutambui," alilalamika.

Kisela pia alisema njia zote muhimu za daladala ndani ya Jiji la Arusha zimeingiliwa na bajaji. Ni kitendo alichokitaja 'siyo sawa' kwa kuwa shughuli za bajaji zinapaswa kufanywa nje ya mji kwa mujibu wa sheria na utaratibu wa Mamlaka ya Udhibiti na Usafiri Ardhini (LATRA).

Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Arusha, Amani Mwakalebela, alikiri mkoa huo kuzidiwa na bajaji na aliahidi kutafuta ufumbuzi wa mgomo huo.

Alisema walitoa leseni kwa bajaji 350, lakini hadi sasa kuna bajaji zaidi ya 3,000 ambazo nyingine hawajui utaratibu wake na wanafanya kazi kinyume cha sheria.

Alisema: "Tunakiri kwamba tumezidiwa na bajaji kwa kuwa zimekuwa nyingi kupita kiasi lakini tunakwenda kufanyia kazi suala hili kwa kulitafutia ufumbuzi."

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, alisema walitoa maelekezo kwa bajaji zinazokiuka utaratibu zikamatwe.

# LATRA yabaini shida mabasi ya Kampuni ya New Force

## ●Kuchunguza ajira za madereva wao

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imesitisha ratiba za safari za saa tisa na saa 11 alfajiri kwa mabasi 38 ya Kampuni ya New Force.

Mkoani Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, aliwaambia waandishi wa habari kuwa sababu ya kuondolewa mabasi hayo katika ratiba hizo za alfajiri ni kutokana na uvunjaji wa makusudi wa kanuni za usafirishaji wa magari ya abiria ikiwamo mwendokasi, kuchezea mfumo na ajali.

"Kampuni ya New Force ni miongoni mwa watoa huduma waliopewa ratiba za saa tisa na saa 11 alfajiri na walipewa sharti la kuhakikisha madereva watakaoendesha mabasi kwa ratiba hizo ni wale waliothibitishwa na LATRA. "Uchunguzi tulioufanya katika magari haya yaliyopata ajali, ulibaini kuwapo kwa uvunjaji wa makusudi wa kanuni za usafirishaji wa magari ya abiria hususani za ratiba za tisa na 11 alfajiri bila dereva kuwa amethibitishwa na mamlaka husika na hata kama amethibitishwa lakini hatumii mfumo wa utambuzi wa dereva (i-button) anapoendesha basi licha ya kanuni kumtaka kuutumia," alifafanua.

Alisema kati ya mabasi hayo 38 ya kampuni hiyo yaliyopewa rukhusa kutoa huduma kwa ratiba za alfajiri, 10 yalipewa rukhsa kwa safari za kuanzia saa tisa usiku na 28 za kuanzia saa 11 alfajiri lakini walibaini kukiukwa masharti waliyotoa ikiwa ni pamoja na kuingiza mabasi ambayo hayakuwa katika ratiba hiyo ya alfajiri.

"Tumebaini ukiukwaji wa ratiba za mabasi ambayo hayakuwa katika ratiba hiyo ya alfajiri ambayo yalikuwa yanatoa huduma katika muda huo bila kibali cha LATRA.

"Pia walikuwa wanachezea mfumo na hata kwenye mabasi yaliyopata ajali hivi karibuni, tumebaini ukiukwaji wa masharti hayo," alisema Suluo.

Alibainisha kuwa mamlaka hiyo imepanga kufanya uchunguzi katika menejimenti ya kampuni hiyo ili kufahamu mfumo wanaotumia kuajiri madereva na wanavyowasimamia.

Pia alisema mamlaka hiyo imeielekeza kampuni hiyo kuwasilisha orodha ya madereva wake wote na namba zao za leseni.

"LATRA iliwahi kusitisha leseni za mabasi sita ya kampuni hii kutokana na madereva wake kukithiri katika ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani.

"Mamlaka ilielekeza madereva wote wa kampuni hiyo kurudi darasani na walitekeleza lakini tunaitaka kampuni iwasilishe tena orodha ya madereva wake na namba zao za leseni kwa uchunguzi zaidi.

"Kwa ujumla mamlaka ipo kwa ajili ya kuwasaidia wawekezaji hawa kukuza mitaji yao na kuendelea kutoa huduma hizi kwa ufanisi na kwa usalama zaidi kwa sababu kwa siku za hivi karibuni tumeshuhudia ajali za mabasi ya abiria ya masafa marefu ambazo zimesababisha madhara madogo na makubwa kwa abiria.

"Ndani ya wiki nne kati ya Juni 6 mpaka Julai 2, mabasi ya kampuni hii ya New Force yamehusika katika ajali tano," alifafanua.

---

TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICES LIMITED

# PUBLIC NOTICE


MR. MOSES VICENT MOSES


MR. TUMAINI MERISY

We would like to inform our stakeholders and the General public that **Mr. Moses Vicent Moses & Mr. Tumaini Merisy** are no longer employed with Tujijenge Tanzania Financial Services Limited

For official communication with Tujijenge Tanzania Financial Services Limited please contact **+255 739 611 611/+255 739 611 612**

---

**CHINA CONSTRUCTION FRONT GROUP (TANZANIA) COMPANY LIMITED S.L.P 101961 DAR ES SALAAM**

**NAMBA YA USAJILI: 139183002**

**TAARIFA YA KUFUNGA KAMPUNI KWA HIARI**

**(Chini ya Kifungu cha 334 (1) cha Sheria ya Makampuni Na. 12 ya (2002)**

Inatolewa taarifa kwa Umma kwamba mnamo tarehe 1 mwezi Januari, 2023 kampuni ya **CHINA CONSTRUCTION FRONT GROUP (TANZANIA) COMPANY LIMITED** ilifikia uamuzi wa kuifunga kwa hiari.

Taarifa inatolewa kwamba **BENO AUSEBIO KINYAMAGOHA** ameteuliwa kuwa Mfilisi wa kampuni.

Wadau wote wa Kampuni hii mnaombwa kutoa taarifa za kina juu ya madai yenu katika anwani iliyotolewa hapo chini ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kuchapishwa Tangazo hili.

Imetolewa Dar es Salaam leo tarehe 1 mwezi Januari, 2023.

**BENO AUSEBIO KINYAMAGOHA, (MFILISI)**
**S.L.P. 34359 - DAR ES SALAAM**
**Bagamoyo road, Victoria, Noble Center 5th Floor**
**SIMU: +255753614256**
**EMAIL: bennoausebio@gmail.com**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**CHAMA CHA MAJAJI NA MAHAKIMU TANZANIA (JMAT)**

# TAARIFA KWA UMMA

Mnamo tarehe 26 Juni, 2023 mfanyabiashara Bw. Rostam Azizi wakati akiongea na vyombo vya habari kuhusu masuala ya uwekezaji alinukuliwa akiituhumu aliyoita Mahakama ya Kisutu kwa kutokuwa huru katika uendeshaji wa shughuli zake.

Kutokana na taarifa hiyo tunapenda kuuhabarisha umma yafuatayo:

Hakuna Jaji anayehudumu katika Mahakama hiyo kama ilivyoripotiwa na mzungumzaji wa taarifa hiyo.

Mahakama ya Tanzania ni chombo pekee cha utoaji haki nchini kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na huendesha shughuli zake kwa uhuru bila kuingiliwa na mtu au chombo chochote.

Uongozi wa Mahakama na au Chama Cha Majaji na Mahakimu haujawahi kupokea tuhuma au lalamiko lolote kutoka kwa mtu yeyote ikionyesha Maafisa wa Mahakama kupigiwa simu na kuelekezwa namna ya kutoa maamuzi katika mahakama hiyo.

Kutokana na maelezo hayo Chama cha Majaji na Mahakimu Tanzania tunatoa kauli zifuatazo;

i) Tumesikitishwa sana na kauli za Bw. Rostam Aziz ambaye hatukutegemea aongee mambo mazito kama hayo bila kuwa na uhakika wala uthibitisho.
ii) Matamshi ya Bw. Rostam Aziz yanaweza kuhatarisha uhusiano na ushirikiano katika mihimili mitatu ya dola ndani ya nchi yetu.
iii) Tunaomba wananchi wenye nia njema na Mahakama na mihimili mingine waendelee kuwa na Imani na mfumo wa utoaji haki nchini.

Kwa taarifa hii, Chama Cha Majaji na Mahakimu Tanzania kinamtaka Bw. Rostam Azizi athibitishe kauli yake akibainisha jina la Jaji na lini alipewa maagizo na Kiongozi wa Serikali kutoa maamuzi kinyume na taratibu zilizopo.

Akishindwa kutoa uthibitisho tunamtaka atumie Jukwaa lile lile kuomba radhi kwa uzito ule ule.

Imetolewa na:

**UONGOZI WA CHAMA CHA MAJAJI NA MAHAKIMU TANZANIA (JMAT)**

**3 JULAI 2023**

# Ajali ilivyoua wanne akiwamo bwana, bibi harusi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WATU wanne wa familia moja akiwamo bwana na bibi harusi, wakazi wa Kijiji cha Lupaso, wilayani Masasi, wamefariki dunia papo hapo kwa kugongwa na Fuso, wakati wakitoka kwenye sherehe ya kufunga ndoa wakiwa wamepakizana staili ya mshikaki kwenye bodaboda.

Akithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Loutery Kanoni, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 1:30 usiku katika barabara ya Newala eneo la Napupa maarufu Anna Abdallah.

Waliofariki katika ajali hiyo wametajwa kuwa ni bwana harusi, Danford Milanzi (29), bibi harusi, Norah Mrope (22), Rashford Milanzi (6) na Omega Danford (23).

Kanoni alisema, lori hilo lenye namna za usajili T 522 BBQ aina ya Fuso, liliwagonga watu hao waliokuwa wamepanda kwenye pikipiki moja.

Alisema Serikali ya Wilaya ya Masasi imepokea kwa masikitiko taarifa ya vifo hivyo na imetoa pole kwa wafiwa, ndugu na jamaa.

Akizungumza na gazeti hili jana, nje ya jengo la kuhifadhia maiti la Hospitali ya Mji Masasi Mkomaindo, kaka wa marehemu, Oliva Haule, alisema taarifa ya vifo vya ndugu zao kwa ajali ya kugongwa na gari walizipokea zikieleza kuwa walikuwa kwenye pikipiki wakitoka mjini Masasi kuelekea kijijini Lupaso.

Mjomba wa marehemu hao, Maxi William, alisema familia yao imekutwa na msiba mkubwa baada ya ndugu zao kupoteza maisha wakati wakitoka kwenye sherehe ya ndoa na kusababisha bibi harusi na bwana harusi, wote kupoteza maisha papo hapo.

Alisema walipopokea taarifa hiyo walikwenda katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji Masasi, Mkomaindo na kushuhudia miili yao ndugu zao.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Emmanuel Sabasi, alithibitisha kupokea miili ya watu wanne wa familia moja waliofariki kwa kugongwa na gari. Alisema walipokea miili hiyo minne juzi ikiwa na majeraha makubwa yaliyosababisha kupoteza maisha yao.

Hata hivyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Nicodemus Katembo, hakupatikana kuthibitisha kutokea kwa ajali hiyo.

## Wakili afungua kesi ya kupinga Jaji Mkuu kuwa ofisini hadi sasa

**Na Grace Gurisha**

SAKATA la Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma kuongezwa muda, limechukua sura mpya baada ya Wakili wa Kujitegemea, Humphrey Malenga kufungua kesi ya kikatiba Mahakama Kuu Masjala Kuu, Dar es Salaam kutaka mahakama hiyo itoe tafsiri ya ibara za kikatiba kuhusiana na ukomo wa nafasi hiyo.

Malenga amefikia hatua hiyo chini ya hati ya dharura kutokana na taarifa zinazosambaa mitandaoni kuwa jaji huyo amestaafu tangu Juni 15, 2023 lakini hadi leo yupo ofisini kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Wakili amefungua kesi hiyo namba 7/2023 dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), akiomba mahakama hiyo itoe tafsiri ya juu ya vifungu au Ibara ya 118 pamoja na Ibara ya 120 (1)(2)(3) ya Katiba, ili kuonesha nafasi ya Jaji Mkuu wa Tanzania.

Baada ya Malenga kufungua kesi hiyo Juni 28, 2023, katika mahakama hiyo, jopo la mawakili wake, Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge na Joyce Brown walipata hati za wito za mahakama na kuziwasilisha kwa AG.

Kesi hiyo ilitajwa jana kwa mara ya kwanza mbele ya Jaji Godfrey Isaya wa mahakama hiyo, Mawakili wa Serikali Alice Mturo na Bavoo Junus wakiomba wapewe muda ili wawasilishe kiapo kinzani dhidi ya kilichowasilishwa na Malenga.

Jaji Isaya aliwataka upande wa Jamhuri kuwasilisha majibu yao Julai 6, mwaka huu na kama kuna jambo ambalo Malenga atataka kuliwasilisha, basi ataliwasilisha mahakamani hapo Julai 10, mwaka huu na kesi itatajwa Julai 11, 2023.

Lipa kwa halopesa



Ada za wateja

| Kiwango (TSH) Range (TSH) | | Tuma HaloPesa Send to HaloPesa | Tuma Kwenda Mitandao Mingine Send to HaloPesa | Tuma Kwenda Namba Isiyosajiliwa Send to Unregistered Number | Kutoa Pesa Withdraw | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kutoka From | Mpaka To | Makato ya HaloPesa HaloPesa Fee | Makato ya HaloPesa HaloPesa Fee | Makato ya HaloPesa HaloPesa Fee | Makato ya HaloPesa HaloPesa Fee | Tozo ya Serikali Govn Levy | Jumla ya Makato Total Fee |
| 100 | 999 | 10 | 10 | - | - | 10 | 10 |
| 1,000 | 1,999 | 25 | 40 | 350 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 25 | 40 | 380 | 330 | 10 | 340 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 80 | 475 | 440 | 14 | 454 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 85 | 530 | 600 | 27 | 627 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 178 | 710 | 845 | 54 | 899 |
| 7,000 | 9,999 | 140 | 180 | 790 | 900 | 56 | 956 |
| 10,000 | 14,999 | 230 | 480 | 1,250 | 1,300 | 102 | 1,402 |
| 15,000 | 19,999 | 240 | 490 | 1250 | 1,400 | 195 | 1,595 |
| 20,000 | 29,999 | 260 | 520 | 1,550 | 1,650 | 306 | 1,956 |
| 30,000 | 39,999 | 270 | 600 | 1,620 | 1,800 | 351 | 2,151 |
| 40,000 | 49,999 | 280 | 648 | 1,800 | 2,100 | 419 | 2,519 |
| 50,000 | 99,999 | 580 | 900 | 2,350 | 2,500 | 573 | 3,073 |
| 100,000 | 199,999 | 700 | 1,350 | 2,750 | 3,300 | 707 | 4,007 |
| 200,000 | 299,999 | 750 | 1,620 | 4,200 | 4,500 | 821 | 5,321 |
| 300,000 | 399,999 | 950 | 1,800 | 5,600 | 5,500 | 838 | 6,338 |
| 400,000 | 499,999 | 1,200 | 1,980 | 6,600 | 6,000 | 982 | 6,932 |
| 500,000 | 599,999 | 1,300 | 2,520 | 7,500 | 6,400 | 1,245 | 7,645 |
| 600,000 | 699,999 | 1,400 | 2,880 | 7,600 | 7,000 | 1,532 | 8,532 |
| 700,000 | 799,999 | 1,400 | 2,880 | 7,650 | 7,000 | 1,700 | 8,700 |
| 800,000 | 899,999 | 1,750 | 3,150 | 8,100 | 7,500 | 1,750 | 9,250 |
| 900,000 | 1,000,000 | 1,750 | 3,150 | 8,300 | 7,500 | 1,776 | 9,276 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 3,000 | 3,600 | 8,300 | 7,500 | 1,875 | 9,375 |
| Zaidi ya 3,000,000 | | 3,000 | 4,500 | 8,300 | 7,500 | 2,000 | 9,500 |

MAZUNGUMZO MAALUM

# Tundu Lissu: Slaa aje, hajafukuzwa

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amemkaribisha aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Wilbroad Slaa, kujiunga nao baada ya kujiondoa miaka minane iliyopita.




Dk. Slaa, mgombea Urais wa Tanzania kwa tiketi ya CHADEMA mwaka 2010, alitangaza kujiondoa katika chama hicho wakati wa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 baada ya kutofautiana kuhusu kumpokea mwanasiasa mzoefu Edward Lowassa kuwa mgombea urais kupitia chama hicho mwaka huo.

Katika mazungumzo na Nipashe nyumbani kwake Tegeta mkoani Dar es Salaam juzi asubuhi, Lissu alisema Dk. Slaa hakuwahi kufukuzwa CHADEMA, hivyo akitaka kurejea, anakaribishwa bila masharti yoyote.

"Dk. Slaa hakuwahi kufukuzwa CHADEMA, hajawahi kufukuzwa kabisa, alijiondoa mwenyewe kwa mambo yake na (Dk. John) Magufuli. Hayo anayajua yeye, lakini hakufukuzwa na chama.

"Katika katiba yetu ya chama, kuna kifungu kinachoruhusu mwanachama aliyefukuzwa kurudi kwenye chama, huyo ni aliyefukuzwa. Sasa Dk. Slaa ambaye alijiuzulu mwenyewe, kama akitaka kurudi sisi tutamzuiaje?

"Hatukuwahi kumfukuza. Kwa hiyo, akitaka hata leo anakaribishwa. Ni tofauti na tuliowafukuza ambao pia na wao wanaweza wakarudishwa. Utaratibu wao ni mgumu kidogo lakini wanaweza wakarudi. Sasa huyu ambaye wala hatukumfukuza, nafasi yake si ni rahisi zaidi!" Alisema.

Dk. Slaa baada ya kujitoa CHADEMA, alimuunga mkono mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Magufuli. Baadaye aliteuliwa na Rais Magufuli kuwa Balozi katika nchi mbalimbali ikiwamo Sweeden, nafasi aliyoitumikia kwa miaka mitano.

Hivi karibuni ameonekana kuwa na msimamo unaoshabihiana na wa CHADEMA katika mambo mengi, hata kupanda jukwaa la chama hicho wilayani Karatu, jambo lililoibua hisia - anataka kurejea katika chama hicho.

**MARIDHIANO**

Kuhusu maridhiano ya CHADEMA, CCM na serikali, Lissu alisema kuwa mpaka sasa hajaona dalili wala mwelekeo mzuri wa jambo hilo, huku akikanusha kutofautiana na Mwenyekiti wa chama chao, Freeman Mbowe.

Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alidai kuwa pamekuwapo maneno zaidi kuliko vitendo, akisisitiza kuwa tangu wakae vikao vya maridhiano, hakuna suala hata moja lililotekelezwa kati ya mambo waliyokubaliana ikiwamo kupatikana katiba mpya.

"Katika suala la maridhiano, maneno ni matamu zaidi kuliko vitendo, watu wanazungumza maridhiano huku wananoa mapanga ya vita.

"Kitu ambacho mimi ninakizungumza hadharani ni kwamba kuna kila dalili tunadanganywa. Ukiangalia kwa macho ya kawaida bila kuvalishwa miwani, utaona kwamba CCM hawataki maridhiano.

"Sikiliza, tunapozungumza maridhiano, unajua tunazungumza vitu gani? Ni kuhusu katiba mpya. Sasa CCM hawataki katiba mpya kabisa. Kwa maneno yao wanaonekana kama wanataka lakini kwa matendo hawataki kabisa.

"Hawataki kubadilisha chochote katika mfumo wa uchaguzi na hiyo wameisema kwa kutumia kile kikosi kazi chao kwamba eti mfumo wetu wa uchaguzi hauna shida," alidai Lissu.

Mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki, alisema sheria zote zinazolalamikiwa kuhusu uchaguzi na tume ya uchaguzi hazijabadilishwa hata moja licha ya kufanyika uchaguzi mdogo katika maeneo mengi nchini na badala yake zimeongezwa zingine alizodai ni mbovu zaidi. Ni jambo analolitaja ni mwelekeo mbaya katika suala la maridhiano.

**STAHIKI ZAKE**

Kuhusu kulipwa stahiki zake, kikiwamo kiinua mgongo cha ubunge na malipo ya matibabu, Lissu alidai ameambiwa tu amelipwa lakini hakuna fedha iliyoingia katika akaunti yake licha ya awali kuahidiwa kuwa angelipwa fedha zote.

"Rais aliniambia nimwandikie barua ya madai yangu na nimemwandikia tangu mwezi Septemba mwaka jana na kuambatanisha risiti zote, nimeambatanisha pia nyaraka za Bunge zinazoonyesha mbunge anayeumwa na kutibiwa nje sheria inasemaje na kanuni za Bunge zinasemaje.

"Kuna nyaraka ambazo zimekuwa zinatolewa kila Bunge jipya linapoanzishwa, zinazoweka utaratibu wa namna ya kuwatibu wabunge nje, nimeambatanisha vyote vile, nimepeleka tangu Septemba mwaka jana na mpaka sasa hivi sijasikia lolote.

"Walicholipa na ambacho nilikisemea walilipa sehemu kidogo tu ya kiinua mgongo changu, siyo yote. Nilitakiwa nilipwe kiinua mgongo cha miezi takriban 44, waliokaa miezi 60 wameniambia kuwa walilipwa Sh. milioni 272 ikiwa na maana kwamba kwa kila mwezi waliotumikia walilipwa kama Sh. milioni nne na ushee hivi. Kwa hiyo, kama hiyo ni kweli, nilitakiwa nilipwe hiyo Sh. milioni nne mara miezi 44," alidai Lissu.

Lissu alisema aliambiwa amelipwa Sh. milioni 79 ambazo hata hivyo hazikuingia katika akaunti yake, bali zililipwa madeni yake ya benki kipindi akiwa mbunge ikiwamo mkopo wa kununua gari ambao hapo awali mkopo huo ulikuwa unalipwa kwa mshahara wake huku kiasi kilichobaki akiwa hajalipwa kabisa.

Kuhusu matibabu yaliyochukua miaka miaka miwili ndani ya na nje ya nchi, Lissu alisema anadai Sh. milioni 400 ambazo ni posho za kibunge, gharama za matibabu na posho ya msaidizi wake aliyekuwa anamwuguza akiwa hospitalini. Zipo kwa mujibu wa sheria.



MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maonesho ya Sabasaba yawe chachu kujifunza

**MAONESHO** ya kimataifa ya kibiashara yaliyoanza mwishoni mwa wiki iliyopita yamewakutanisha wafanyabiashara kutoka mataifa mbalimbali duniani ili kuonesha bidhaa zao na vile vile kutafuta soko katika nchi nyingine.

Maonesho hayo yasichukuliwe kama sehemu ya kwenda kutembea, bali wananchi wapate fursa ya kujifunza mambo mbalimbali yanayooneshwa kwenye mabanda ya wafanyabiashara hao.

Maonesho hayo pia yanatoa fursa kwa wajasiriamali hasa mamalishe kuwa na mabanda yao kwa ajili ya kuwahudumia chakula wanaokwenda kwenye maonesho hayo na vile vile kujipatia kipato.

Baadhi ya watu wanaokwenda kuangalia maonesho hayo, lengo lao ni kwenda kununua bidhaa ambazo zingine huuzwa kwa bei nafuu.

Lakini, lengo la maonesho hayo ni kutoa fursa kwa wafanyabiashara wa ndani, wananchi kujifunza kwa wenzao na kutafuta soko na vile vile ni njia ya kutengeneza mawasiliano ili wanapotaka kutembelea nchi zingine kujifunza zaidi iwe rahisi kwao.

Taasisi, mashirika, viwanda, kampuni pia hupata fursa ya kuonesha huduma wanazozitoa kwa wananchi na kuwarahisishia wanapokwenda kutembelea mabanda yao.

Vyuo vya elimu ya juu pia hutoa huduma ya kuelimisha vijana wanaopenda kuendelea na vyuo vikuu namna ya kujiunga na vyuo hivyo.

Maonesho hayo siyo kwa ajili ya kuonyesha bidhaa pekee bali kuna mambo mbalimbali ya kujifunza na mtu anapotoka huko anakuwa amepata elimu na maarifa.

Kuna mabanda ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ambayo huwa ni kivutio kikubwa cha wananchi kutokana na bidhaa zao zikiwamo samani za ndani ambazo hutengenezwa kwa ubora wa hali ya juu pamoja na bustani za mboga zinazooteshwa kwa utaalamu.

Katika banda hilo watu hujifunza jinsi ya kulima bustani katika eneo dogo ambalo linaweza kumfanya mtu kupata mazao mengi na vile vile jinsi ya kufuga kisasa.

Kwa wale ambao hawajawahi kutembelea mbuga za wanyama, kwenye maonesho hayo wanapata fursa ya pekee ya kuwaona wanyama kama simba, chui, swala na wengine tena kwa kushuhudia kwa macho.

Ni kipindi kizuri pia cha wazazi kuwapeleka watoto wao kwenda kujifunza mambo mbalimbali yaliyopo kwenye maonesho hayo.

Wanafunzi wa vyuo vikuu pia wanaonesha bunifu zao kwa kutumia vipaji vyao na kutoa fursa kwao kujitangaza na kupata ajira au kujiajiri.

Ki ukweli maonesho hayo yana mambo mengi ya kujifunza na pia hukutanisha Watanzania na wenzao wa mataifa mbalimbali.

Bidhaa zinazotengenezwa Tanzania ni wakati wake wa kujitangaza na kupata soko katika nchi zingine duniani.


Watanzania wana uwezo mkubwa wa kutengeneza bidhaa zenye ubora, lakini wanakosa elimu ya kujitangaza kama waliyonayo wenzetu wa nchi jirani.

Huu ni wakati wa Watanzania wazalishaji kutengeneza kadi za mawasiliano na vipeperushi vya kujitangaza ili waweze kujulikana.

Sasa dunia inakwenda kidijitali, bidhaa zinauzwa kwa mtandao, hivyo ni rahisi bidhaa kutoka Tanzania ikauzwa Ulaya na pesa pia ikatumwa kwa njia ya mtandao bila kupata usumbufu wa kusafiri na kutumia gharama kubwa.

Hivyo, Watanzania tutumie maonesho haya kwa ajili ya kutafuta fursa za kibiashara na vile vile, kujifunza toka kwa wenzetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Kasi ingeongezwa mafunzo ya matumizi ya vishikwambi

**WALIMU** 33 wa shule za sekondari wilayani Temeke, mkoa wa Dar es Salaam wamepata mafunzo ya jinsi ya kutumia vishikwambi vilivyotolewa na serikali kwa lengo la kuboresha kazi ya ufundishaji.

Juni 12 hadi 22 mwaka huu, walimu hao walikuwa wanapata mafunzo yaliyotolewa na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kama kichocheo kwa walimu kuendana na mageuzi na maendeleo ya viwanda.

Huku walimu hao 33 wa shule za sekondari wakiwa wamefundishwa, wengine 49 wa shule za msingi wilayani humo nao wanatarajia kupata mafunzo kama hayo kuhusu matumizi ya vishikwambi.

Wakati walimu hao wakipata mafunzo hayo, mengine yalikuwa yakiendelea kutolewa katika mikoa ya Arusha na Ruvuma, ili kuhakikisha wanaingia katika teknolojia ya kisasa.

Kanda ya Ziwa, walimu 200 wa jijini Mwanza nao wamefaidika na mafunzo hayo ya kutumia vishikwambi, huku mikakati ya kuelimisha walimu kwa wilaya zote za Tanzania, ikiendelea.

Binafsi ninaunga mkono juhudi hizo za kuwapa mafunzo walimu kuhusu matumizi ya vishikwambi, lakini ninafikiri ni vyema utoaji wa mafunzo hayo ukawa wa nchi nzima ili asiwapo mwalimu ambaye hajafundishwa.

Siyo siri kwamba mafunzo hayo yanatokana na kuwapo kwa pengo kwa walimu kuhusu matumizi ya vifaa hivyo, kwani hata wao waliwahi kukiri na kuomba kufundishwa matumizi yake.

Hatua ya serikali kugawa vishikwambi ililenga kuboresha mazingira ya ufundishaji na matumizi ya teknolojia kwa kuwa vikitumiwa ipasavyo, vinawezesha utoaji wa elimu bora.

Kwa ujumla, vishikwambi vinaweza kutumika kufundishia, kuwasilisha taarifa za kufundishia, kutafuta taarifa mitandaoni na hata kuchakata taarifa za matokeo ya wanafunzi.

**Hatua ya serikali kugawa vishikwambi ililenga kuboresha mazingira ya ufundishaji na matumizi ya teknolojia kwa kuwa vikitumiwa ipasavyo, vinawezesha utoaji wa elimu bora.**

Ninafikiri ni muhimu walimu kuendelea kujifunza masuala mbalimbali kuhusu TEHAMA kwa ajili ya kupata maarifa ambayo yatawasaidia katika kazi ya ufundishaji.

Serikali kwa upande wake, imejitahidi kuwarahisishia kazi ya ufundishaji, hivyo jambo muhimu ni kusambaza mafunzo ya matumizi ya vifaa hivyo na kuhakikisha kila mwalimu anayapata.

Mendeleo yamesababisha kuenea kwa lugha zinazotumika katika teknolojia hiyo, ndiyo maana unakuwapo umuhimu wa kuwapa mafunzo walimu ili waelewe matumizi ya vishikwambi walivyopewa.

Ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA umekuwa ukifanyika kwenye masomo mbalimbali kama vile ya sayansi na ya sanaa, inaelezwa umekuwa ukitoa matokeo chanya.

TEHAMA ni kiungo muhimu katika maendeleo ya watu duniani, kwani wamekuwa wakitumia teknolojia hiyo katika kufanya mawasiliano pia, hivyo wigo uendelee kupanuliwa ili kuwafikia walimu wote.

Ninaamini kuwa walimu nao wanatakiwa kuendana na wakati, ili wasipitwe na wakati kwa kuwa kizazi cha sasa hususan watoto wenye umri mdogo, baadhi yao wana uwezo wa kutumia simu janja au vifaa vya kielektroniki kuliko wazazi wao, bila mafunzo ya matumizi.

Si vyema watoto wadogo kujua kutumia simu janja au vifaa vya kielektroniki, huku mwalimu akiwa hajui. Mafunzo kwa walimu yanayoendelea kutolewa, yasambae kote na yawe na matokeo chanya.

# Hasira, chuki dalili mtu kuwa tatizo afya ya akili

**Na Gwamaka Alipipi**

HASIRA, chuki ya muda mrefu vimetajwa kuwa mojawapo ya dalili ya mtu mwenye tatizo la afya ya akili, na inaweza kutibika kwa mwathirika kupewa elimu na ushauri sahihi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Familyvibes, Dk. Mayrose Majinge, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusu maandalizi ya kongamano tiba la kitaifa la afya ya akili litakalofanyika Julai 11, mwaka huu, katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Dk. Mayrose alisema kuna dalili nyingi za mtu mwenye tatizo la afya duni ya akili na baadhi ya visababishi ni hali ya umaskini, njaa.

"Utakuta mtu anamchukia mwenzake kwa muda mrefu, au anakuwa na hasira ya mara kwa mara. Hiyo ni mojawapo ya dalili ya mtu mwenye tatizo la afya ya akili. Sisi tunachokifanya tunatoa elimu kwa jamii kwa makundi na mtu binafsi kuhusu namna ya kudhibiti hali hiyo," alisema Dk. Mayrose.

Alisema ili mtu awe na afya bora ya akili anapaswa kula chakula bora hali itakayosababisha kupata mawazo yenye tija ambayo yatamnufaisha katika maisha yake ya kila siku.

Kuhusu kongamano, Dk. Mayrose alisema litabeba kaulimbiu: 'Dhibiti magonjwa yako kwa afya ya akili' na litawakutanisha wataalamu wa afya kutoka maeneo mbalimbali ya nchi.

Alisema mgeni rasmi katika kongamano hilo anatarajia kuwa Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Mohamed Janabi.

Dk. Mayrose alisema lengo kuu la kongamano hilo ni kutengeneza uelewa na nguvu ya taifa namna ya kukabiliana na changamoto ya magonjwa ya afya duni ya akili.

"Kwa hiyo katika kongamano hilo watu watapata fursa ya kupima afya kwa sababu madaktari bingwa kutoka hospitali mbalimbali hapa nchini watakuwapo. Hivyo tunawakaribisha watu wote waje kwa wingi," alisema Dk. Mayrose.

Kadhalika, alitoa rai kwa serikali kuwa na sera katika mitaala ya elimu kuanzia hatua ya chekechea hadi elimu ya juu, somo la afya duni ya akili litafundishwa kama masomo mengine.

Alisema kwa kufanya hivyo itasaidia kupeleka uelewa wa tatizo la afya duni ya akili katika jamii na kuondoa dhana potofu na mtu mwenye afya ya akili ni lazima awe amechanganyikiwa.



Ofisa Elimu wa Shule za Msingi wilayani Muheza mkoani Tanga, Pili Maxmilian, akizungumza na waandishi wa habari juzi, alipotoa taarifa ya hali ya elimu msingi na sekondari katika ujenzi wa vyumba vya madarasa, vyoo na nyumba za walimu baada ya serikali kupeleka fedha wilayani humo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mwinyi apongeza uhusiano mzuri wa Tanzania, China

**Na Mwandishi Maalum**

HUKU dunia ikikabiliwa na changamoto kama mivutano ya kisiasa na mabadiliko ya tabianchi, Afrika na China zitaendelea kuwa na uhusiano wa karibu na kusaidiana, Rais wa Tanzania Zanzibar, Hussein Ali Mwinyi amesema katika mahojiano na Shirika la Habari la China, Xinhua Jumamosi iliyopita.

"Tumekuwa na ushirikiano mzuri tangu nyakati za kihistoria," alisema Mwinyi ambaye amekuwa ziarani nchini China kushiriki kwenye maonyesho ya tatu ya Uchumi na Biashara ya China na Afrika yaliyofanyika kuanzia Alhamisi hadi Jumapili, iliyopita.

Kwa miongo kadhaa, pande hizi mbili, "kama washirika wa karibu sana," zimeshuhudia "kutobadilika" katika kujitolea kwao kusaidiana, alisema Rais Mwinyi.

"Kwa bahati nzuri, tumekuwa karibu sana na China...sera zetu zinaendana na tutaendelea kufanya kazi na China," amesisitiza.

Rais Mwinyi amesema, kuimarika kwa uchumi wa China baada ya janga la UVIKO-19 kumeleta fursa nyingi na kuingiza nguvu katika uchumi wa Afrika.

"Kwa kuona kwamba baada ya janga hili, mambo yanarudi katika nyakati za kabla ya janga (nchini China), tunafurahi kuwa hapa kuona kwamba tunafanya mambo ya maendeleo tena," alisema.

Rais Mwinyi alisema, Tanzania ni nchi ya kilimo na kupitia uwekezaji katika miundombinu na maeneo maalum ya viwanda, China inaipatia nchi hiyo uwezo wa kutengeneza mazao ya kilimo na kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani ya mazao jambo ambalo ni muhimu.

> **"Kwa bahati nzuri, tumekuwa karibu sana na China... sera zetu zinaendana na tutaendelea kufanya kazi na China," amesisitiza.**

"Nchi za Afrika zinataka kuwa na uwezo wa kujitegemea," alisisitiza Rais Mwinyi na kuongeza kuwa ushirikiano na China una umuhimu mkubwa kwao ili kufikia lengo hilo na kujenga hali yenye manufaa kwa pande zote mbili.

Akizungumzia hisia zake kwa China wakati wa ziara hiyo, Rais Mwinyi alisema kuwa amefurahishwa na mafanikio yaliyopatikana nchini China: Miundombinu na maendeleo, na uboreshaji wote wa uchumi.

"China inatoa mifano inayofaa kuigwa katika bara la Afrika," Mwinyi alisema. "Tunaona kuna kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi, lakini pia tunaona mafanikio mengi katika sekta zote."

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Mhitimu VETA atengeneza kifaa kuchakata matunda

**Na Beatrice Shayo**

MHITIMU wa Chuo cha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Arusha (VETA), George Nyahende, ametengeneza kifaa kwa ajili ya uchakataji wa matunda na mazao ili kutatua tatizo la upotevu wa mazao kwa wakulima wengi nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam na waandishi wa habari katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Nyerere, alisema mazao mengi yamekuwa yakipotea wakati wa mavuno, mashine hiyo itasaidia kutatua tatizo hilo.

"Wakulima wengi wanapata hasara kipindi cha mavuno kutokana na mazao kuwa mengi na mengine kuoza hali inayosababisha kupoteza mapato yao," alisema na kuongeza;

"Utakuta wakulima wanavuna mazao yao ambayo ni ya msimu na ukizingatia kipindi cha msimu wa matunda yanakuwa mengi hivyo kusababisha mengine kupotea kwa kuharibika na mengine wakulima uamua kuuza kwa hasara kwa kuhofia kuharibika,"

Mashine hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuokoa fedha za wakulima zinazopotea kwani watabadilisha matunda na kuyahifadhi kwa njia ya unga na kuuza katika masoko makubwa.

Alisema mashine hiyo inasaidia kwa kiasi kikubwa mkulima kuuza mazao yake kwa utaratibu ikilinganishwa na awali wanauza kwa hasara kutokana na kuhofia kuharibika.

"Nilishuhudia wakulima wa vitunguu mkoani Arusha, walikuwa wakipata shida hiyo wakivuna vitunguu vyao vingine huwa vinaharibika wakija wanunuzi wanataja bei zao mfukoni hii inakuwa kama wanawanyonya wakulima," alisema.

Alisema wanunuzi hawaangalii gharama ya uandaaji wanajipangia bei zao wenyewe watakapochakata matunda kuwa ya unga yatasaidia kuuza kwa utaratibu na kupata faida.

Nyahende alisema mashine hiyo inauwezo wa kukausha mazao kuanzia kilo 100 hadi tani moja kwa wakati mmoja kulingana na ukubwa wa mashine.



Wakazi mbalimbali wakitoka kununua vitu katika Viwanja vya Biashara vya Kimataifa vya Mwalimu Nyerere Sabasaba jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kampuni China zamiminika Sabasaba

**Na Joseph Mwendapole**

UJUMBE wa wafanyabiashara kutoka kampuni zaidi ya 50 za nchini China zimewasili kwa ajili ya kushiriki maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

Wafanyabiashara hao pia wamekuja kwa ajili ya kuangalia fursa za uwekezaji nchini ambao watakutana na kufanya mazungumzo na wenzao wa Tanzania.

Jumla ya nchi 14 zimethibitisha kushiriki maonyesho hayo yaliyoanza kufanyika kuanzia Juni 28 hadi Julai 14, mwaka huu, kampuni 112 kutoka nje ya nchi na 1,188 za ndani zinashiriki.

Ujumbe huo uliwasili jana asubuhi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere huku ukiahidi kuonesha bidhaa mbalimbali ikiwamo vifaa vya kielektroniki.

Vifaa hivyo ni pamoja na miradi, kompyuta, simu za mkononi na teknolojia mbalimbali mpya ambazo zimebuniwa na zimeshaanza kutumika.

Akizungumza baada ya mapokezi hayo, Kaimu Mkurugenzi Uwekezaji Biashara kutoka Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade), Fortunatus Mhambe, alisema ujio wa ujumbe huo ni matunda ya ushirikiano kati ya Tanzania na China.

Aliseama licha ya kushiriki maonyesho ya mwaka huu pia wafanyabiashara hao wa China watakutana na wenzao wa Tanzania na kuangalia fursa mbalimbali za uwekezaji.

Alisema kampuni hizo zitaonyesha bidhaa zao na huduma mbalimbali ambazo wamekuja nazo hivyo ni fursa kwa watanzania kuangalia namna ya kushirikiana na wawekezaji hao.

"Dunia ilipata changamoto ya Uviko-19 mwaka 2020 kwa hiyo Maonyesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam yalikosa washiriki kutoka nchi mbalimbali hasa China kutokana na zuio la kusafiri kwa wakati huo lakini sasa mambo yamekuwa safi," alisema.

"Hali kwa sasa ni nzuri sana kwasababu mwaka huu tunao washiriki kutoka nchi zaidi ya 16 na wenzetu kutoka China wamechukua banda zima ambalo kunakuwa na washiriki zaidi ya 100 kutoka nchi hiyo kwahiyo mwaka huu yameinuka zaidi," alisema.

Meneja wa Kituo cha Biashara cha Afrika Mashariki, Wang Xiangyu, alisema kupitia maonesho hayo Watanzania watapata fursa mbalimbali na ni muhimu kuwatembelea wafanyabiashara hao.

"Leo tumekuja na kampuni kutoka China kushiriki maonyesho ya Sabasaba ambayo ni maarufu nchini China hivyo kama mnataka kujua tyeknolojia mpya za simu, kompyuta na vifaa vingine vingi karibu Sabasaba," alisema Wang.

# 'Sabasaba iwe fursa kibiashara kwa Watanzania'

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), imesema Watanzania wayachukulie Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, kama fursa ya kujifunza na kufanya uzalishaji wa bidhaa zenye ubora na viwango, kama zile zinazotoka nchi tofauti zinazoshiriki maonesho hayo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Latifa Khamis, amesema, bidhaa zinazooneshwa kutoka nchi tofauti, zinakubalika kimataifa, ndiyo maana zinavuka mipaka na kushiriki maonesho kama hayo.

Latifa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, kwenye maonesho hayo katika maadhimisho ya Siku ya Iran, yaliyofanyika katika uwanja wa Mwalimu. J.K Nyerere, yenye lengo la kutangaza fursa za biashara na uwekezaji zilizopo Iran na Tanzania katika sekta ya utalii, elimu, viwanda pamoja na afya.

Alisema Tanzania imekuwa na uhusiano mzuri kidiplomasia na kiutamaduni na nchi ya Iran kwa zaidi ya miaka 40 hivyo TanTrade, inawahamasisha Watanzania kutumia fursa za biashara na uwekezaji zilizopo nchi ya Iran, pamoja na uwezeshaji wa biashara na nafuu ya gharama za kuendesha biashara.

"TanTrade inaendelea kudumisha uhusiano wa biashara na uwekezaji yaliyoanzishwa na Hayati Baba wa Taifa Mwl. JK Nyerere pamoja na Rais wa zamani wa Iran Ayatollah Khamenei, hivyo kuunga mkono juhudi za serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha uchumi wa nchi unakuwa kwa kasi zaidi.

"Tunatangaza bidhaa za Tanzania na kuvutia uwekezaji katika viwanda vya ndani ya nchi ili kuchochea uzalishaji na kupata masoko ya ndani na nje ya nchi. Natoa wito kwa Watanzania kutumia fursa zilizopo nchini Iran, ili kuongeza mapato kwa mfanyabiashara mmoja mmoja pamoja na kuchochea uchumi wa taifa kwa ujumla," alisema Latifa.

Pia alibainisha maonesho hayo, yatakuwa na mikutano ya kuwaunganisha wafanyabiashara mbalimbali, kukuza uwekezaji wa sekta ya viwanda ili kufanikisha kwa viwango vya juu.

Mwenyekiti wa Bodi ya TanTrade, Ulingeta Mbamba, alisema Iran ziko fursa za utalii, elimu na kilimo, hivyo Tanzania kuzalisha mazao pamoja na madini na kuuza katika soko la nchi hiyo.

"Kwa kipindi hiki cha Sabasaba, Iran wamekuja kujitangaza na kuendelea kuunga undugu wa kibiashara na uwekezaji na Watanzania, hivyo nawaasa Watanzania waichukulie hii kama fursa ya kujifunza uzalishaji wa bidhaa zenye ubora viwango vinavyokubalika kimataifa," alisema Mbamba.

Balozi wa Iran nchini, Hussein Alvandi Behineh, alitoa shukrani kwa serikali, kupitia TanTrade kwa kupata fursa ya kushiriki na kuadhimisha siku ya Iran katika maonesho hayo na kuzitangaza nchi bidhaa wanazozizalisha.

"Tunatoa wito kwa Watanzania kutembelea Sabasaba na pia kutembelea katika banda letu na kujionea bidhaa tofauti, zenye ubora na viwango vya kimataifa pia waje wajifunze fursa za kibiashara zinazopatikana nchini Iran," alisema Balozi Bahineh, akiongeza:

"Tanzania na Iran, inapaswa kuungana na kuwa kitu kimoja katika biashara, ili kuleta uchumi endelevu na wenye afya pamoja na kujenga uhusiano mzuri pamoja na kuinuana katika biashara na uwekezaji."





# Majaji sita Mahakama ya Rufani kusikiliza kesi 65

**Na Mary Mosha,** MOSHI

JOPO la majaji sita wa Mahakama ya Rufani limeanza rasmi vikao vyake vya kusikiliza kesi 65 zilizopangwa na Masjala ya Mahakama Kuu, Kanda ya Moshi.

Naibu Msajili wa Mahakama ya Rufani, Emmanuel Mrang'u, alisema jana kuwa kati ya kesi hizo, 49 ni rufani za madai na 16 ni za jinai.

"Jopo la kwanza la majaji watatu litaongozwa na Jaji Mwanaisha Kwariko na jopo la pili la majaji litaongozwa na Jaji Winfrida Korosso.

"Vikao hivi kwa mujibu wa sheria vinafanyikia katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, kwenye kumbi za wazi namba 1 na namba 2."

Naibu Msajili huyo, alisema vikao hivyo vitafanyika kwa muda wa wiki tatu kuanzia Julai 3, mwaka huu.

Majaji wengine watakaounda jopo la kwanza ni Jaji, Dk. Marycaroline Levira na Jaji Gerson Mdemu watakaosikiliza kesi za rufani 32, wakati jopo la pili litawahusisha pia, Jaji Paul Kihwelo na Jaji Sam Rumanyika, ambao rufani 33.

Alisema lengo la kupeleka kesi hizo za rufani Mahakama Kuu, Kanda ya Moshi ni utekelezaji wa mpango mkakati wa Mahakama ya Tanzania wa mwaka 2020/21-24/25, nguzo namba 2 ya upatikanaji wa haki kwa wakati.

# RC achefuka walimu kuhamishwa ovyo

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

KUHAMA kwa walimu vijijini katika Mkoa wa Manyara, kumemchefua Mkuu wa Mkoa huo, Queen Sendiga na kutangaza marufuku kwa walimu kuhamishwa pasipo kuwapo na mbadala wa kuziba nafasi hiyo.

Pia, ameagiza Katibu Tawala Msaidizi, Sekretarieti ya Mkoa huo, anayeshughulikia elimu (REO), kuhakikisha kunakuwapo na msawazo sawa wa walimu wapya 245 waliopangwa mkoani Manyara.

Sendiga alitangaza marufuku hiyo jana, wakati akizungumza na Nipashe, kuhusu miradi ya elimu na namna serikali inavyouwezesha mkoa huo kuimarisha miundombinu ya elimu.

"Nataka nieleweke vizuri, ni marufuku kuhamisha walimu kutoka katika halmashauri zilizoko pembezoni; hapa namaanisha walimu wa vijijini kuja mjini, kabla ya kupeleka walimu mbadala, kwa ajili ya kuziba hiyo nafasi. Hii itasaidia kuondokana na upungufu wa walimu.

Zaidi alisisitiza, "Nitapita kila halmashauri, kukagua mwenyewe kuona kama kuna msawazo sawa wa walimu waliopangwa mkoa huu."

Pamoja na mambo mengine, Sendiga, alizuia zoezi la kuhamisha walimu, badala yake aliagiza wabaki katika vituo vyao watakavyopangiwa mpaka hapo atakapotangaza vinginevyo.

Kadhalika, alisema tayari wamepokea Sh. bilioni 6.417 ambazo zitatumika kujenga miundombinu ya shule za msingi 44 katika halmashauri saba na shule mpya nane.

Alisema miundombinu hiyo itajengwa kwenye shule moja kwenye halmashauri husika, isipokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, ambayo ina shule mbili mpya.

Alisema fedha hizo zitatumika kuongeza miundombinu mingine katika shule 36, ambapo madarasa yatakuwa 87, mabweni mawili, matundu ya vyoo 90 na nyumba za walimu mbili za kisasa.

Alitaja fedha nyingine ambazo mkoa umepokea ni Sh. bilioni 1.490 ya miradi ya Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) na mradi wa miundombinu ya kidato cha tano kupitia fedha za serikali kuu Sh. bilioni 3.187.

Alitaja mingine ni mradi wa miundombinu ya kidato cha tano kupitia Sh. milioni 186.3 na mradi wa kuboresha elimu ya sekondari Sh. bilioni 4.089.



Mbunge wa Viti Maalum (vyuo vikuu), Dk. Pauline Nahato (kulia), akikumbatiana na Mkuu wa Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, Esta Mahawe, walipokutana kwenye harambee ya kuchangia fedha za ujenzi wa ofisi ya Tanzania Rift Valley Field (TRVF) ya Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA) eneo la Kiongozi Mjini Babati mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Serikali yawatangazia kibano Ma-DED, DC wazembe

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imetangaza kibano dhidi ya wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri za Mkoa wa Arusha, ambao maeneo yao yatabainika kuwa na maendeleo hafifu licha ya kutengewa bajeti nono na serikali.

Hivyo kuanzia sasa watalazimika kusaini mkataba wa ziada wa kusimamia miradi inayotekelezwa katika maeneo yao kwa bajeti iliyopangwa.

Jana, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alipiga marufuku katika mwaka huu wa fedha wa 2023/24, wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo kuchukua fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kumalizia miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa bajeti, lakini inashindikana kukamilika.

Mongella alikuwa akizungumza na madiwani wa Halmashauri ya Arusha, kuhusu utekelezaji wa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu na Serikali za Mitaa (LAAC), kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Kwa mujibu wa Mongella, kwa baadhi ya maeneo miradi hiyo haikumalizika kutekelezwa kutokana na uzembe.

Kabla ya kauli hiyo kutolewa, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, alisema walishakubaliana kwamba ni marufuku kuanza mradi mpya wa mapato ya ndani, kabla ya kumaliza miradi viporo iliyopo.

"Haiwezekani miradi inajengwa tangu mwaka 2017 hadi sasa haikamiliki. Niombe tumalize viporo vyote ndipo tuanzishe miradi mipya," alisema.

Kuhusu miradi ya fedha zinazotoka serikalini, Mtahengerwa, alisema atahakikisha inakamailika kwa bajeti itakayotengwa na kwa ubora unatakiwa.

# Migogoro ya wanyama, binadamu yavitesa vijiji 23

**Na Godfrey Mushi,** SAME

VIJIJI 23 vilivyoko Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, vinakabiliwa na migogoro isiyokwisha kati ya tembo na binadamu kwa zaidi ya miaka minane sasa.

Ofisa wanyamapori wa wilaya hiyo, Thomas Katunzi, alisema jana kuwa migogoro kati ya tembo na binadamu, ambayo imekuwa ikiitesa wilaya hiyo ni ile iliyoanza mwaka 2014 hadi kufikia mwaka 2022.

Kwa mwaka huu (2023), matukio ya tembo kuvamia mashamba na makazi ya watu na kuharibu mazao na mali mbalimbali, yamevitikisa zaidi vijiji vya Mferejini, Darajani, Marwa, Jiungeni, Njoro, Emuguri, Ishinde, Chankonko-Makanya, Kitamri, Kavambughu na Masandare.

"Mwaka 2022, matukio yaliyoripotiwa yalikuwa 17 katika Kata ya Vumari, mazao yaliyoharibiwa ni ekari 56, wakati mwaka 2021, tembo katika kata hiyo hiyo walivamia mara 13 na kuharibu mazao katika ekari 7.5

"Hali ilikuwa mbaya zaidi mwaka 2019, ambapo matukio ya tembo yaliripotiwa 172, huku mazao yaliyoharibiwa yakiwa ekari 219."

Alisema Kata ya Kisiwani, kuliripotiwa matukio ya uvamizi wa tembo 227 mwaka 2021 na waliharibu mazao katika ekari 316.

Kadhalika alisema mwaka 2022, Kata ya Maore, tembo walivamia ekari 325.4 na kuharibu mazao ya wananchi katika matukio 299 yaliyoripotiwa, huku wakijeruhi wananchi wawili na kuua mtu mmoja.


Alisema katika Kata ya Ndungu, tembo walivamia ekari za mazao ya chakula 61 katika matukio 54 yaliyoripotiwa.

Aidha, alisema Kata ya Kalimawe, tembo hao kwa mwaka 2022, walivamia ekari 140 katika matukio 120 yaliyoripotiwa na Kata ya Bendera, tembo walivamia 34.5 katika matukio 67 yaliyoripotiwa.

Kuhusu malipo ya fidia ya kifuta jasho kwa wananchi waliopoteza mazao yao, alisema hadi sasa serikali imelipa zaidi ya Sh. milioni 150 kwa miaka mitatu.

Kwa mujibu wa Msimamizi wa Mradi wa SOKNOT Tanzania ambaye ni mtaalamu mbobezi wa tembo, Prof. Noah Sitati, mradi wanaoutekeleza unalenga kupunguza kwa asilimia 40 migogoro ya tembo na binadamu, ifikapo mwaka 2025.

WWF Tanzania, inatekeleza mradi mkubwa wa SOKNOT katika mikoa ya Tanga na Kilimanjaro, ambao unalenga zaidi kutafuta suluhu ya kudumu ya migogoro, kati ya tembo na binadamu (HEC) katika ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.





# Shilingi bilioni 97 kujenga Barabara ya Kahama-Geita

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 97 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kata ya Busoko Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga hadi Kijiji na Kata ya Bukori mkoani Geita yenye urefu wa kilometa 75.

Barabara hiyo inatarajiwa kuondoa adha ya usafiri na usafirishaji wa madini ya pamoja na mazao ya chakula na biashara ambayo imekuwa ikiwakumba wafanyabiashara na wakulima wa maeneo hayo kutokana na barabara kuwa mbovu.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, hivi karibuni wakati akizungumza na madiwani pamoja na watumishi wa Halmashauri ya Msalala, kwenye mkutano maalum wa Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo.

Alisema serikali imekuwa ikiunganisha mawasiliano ya barabara kila mwaka wa fedha, wilaya hadi mikoa kwa kurekebisha na kuzijenga upya barabara za vumbi kwa kiwango cha lami. Alisema lengo la kufanya hivyo ni kurahisisha mawasiliano na usafirishaji wa bidhaa mbalimbali hadi kwa mtumiaji wa mwisho vijijini.

Mndemea alisema Barabara ya Kahama-Bukori mkoani Geita imetengewa Sh. bilioni 97 kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami na mchakato unaendelea wa kumtafuta mzabuni na utakapokamilika ujenzi utaanza mara moja, huku akiwataka vijana kuchangamkia fursa za ajira za muda pindi ujenzi utakapoanza au kutangazwa.

Pia aliwataka wananchi waliojenga makazi yao ya kudumu ndani ya alama za barabara zilizowekwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) kuchukua hatua za haraka kabla ya kuondolewa ili kuondoa migogoro isiyokuwa na ulazima.

Diwani wa Ikinda, Matrida Musoma, alisema, ubovu wa barabara hiyo umesababisha kuwa na gharama kubwa ya usafirishaji wa mazao hadi sokoni, hivyo ujenzi wake utakapoanza na kukamilika utasaidia kuondoa gharama hizo na wakulima kupata fedha za kuendesha maisha na familia zao.

Mkazi wa Segese Halmashauri hiyo, Kevin Bakari alisema, kwa sasa gunia moja la dengu linasafirishwa kwa Sh. 50,000 hadi sokoni, huku mpunga ukisafirishwa kwa Sh. 1,000 hadi 2,000 na kuiomba serikali kutochukua muda mrefu kutafuta mzabuni ili ujenzi uanze mara moja.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akimkabidhi kompyuta Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Tumbaku cha mkoani Kigoma, Gilbert Makwaya (wa pili kushoto), zilizotolewa na Kampuni ya Tumbaku ya Alliance One, kulia ni Mkurugenzi wa Uzalishaji, David Mayunga na msemaji wa kampuni hiyo, John Magoti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC awaonya sungusungu kuacha vitendo vya ukatili

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, amelitaka Jeshi la Jadi (sungusungu) kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi, kuacha tabia ya kuwafanyia wahalifu vitendo vya ukatili pale wanapowakamata, badala yake wafuate utaratibu na kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Alibainisha hayo juzi kwenye kampeni ya 'Kataa uhalifu toa taarifa, Shinyanga bila uhalifu inawezekana' iliyofanyika katika Kata ya Ndala Manispaa ya Shinyanga chini ya Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga.

Alisema serikali inatambua mchango mkubwa wa jeshi hilo katika kukabiliana na kutokomeza uhalifu, lakini akawazuia tabia ya utoaji wa adhabu kali zilizo kinyume na sheria sambamba na ukatili bali washirikiane na vyombo vingine vya sheria likiwamo Jeshi la Polisi ili kila mmoja apate haki yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, aliwataka wananchi kuachana na vitendo vya uhalifu ikiwa ni pamoja na uvutaji wa dawa za kulevya, bali wajitume kufanya kazi halali ikiwamo kupata ajira katika miradi ya kimkakati ambayo inatekelezwa hapa nchi.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi wa mkoa huo kuendelee kushirikiana na jeshi hilo kwa kutoa taarifa mbalimbali za uhalifu, ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria na kukomesha uhalifu mkoani humo, huku akibainisha kwamba kampeni hiyo ni endelevu.

Kamanda wa Jeshi la Jadi (sungusungu) Manispaa ya Shinyanga, John Kadama, alisema maelekezo yote ambayo yametolewa watayafanyia kazi ikiwamo kushirikiana na Jeshi la Polisi pale watakapowakamata watuhumiwa na kuacha kujichukulia sheria mkononi.

# WAMACU wang'ara shindano ubora wa kahawa

**Na Timothy Itembe** MARA

CHAMA Kikuu cha Wakulima Mkoa wa Mara (WAMACU) kwa mara nyingine kimeibuka kidedea katika mashindano ya kitaifa ya ubora wa kahawa.

Hivyo wamepewa zawadi ya cheti na ngao baada ya sampuli ya zao hilo kutoka mkoani Mara kubainika kuwa bora zaidi kufuatia shindano lililofanywa chini ya Bodi ya Kahawa nchini.

Shindano hilo lilifanyika kwa kuchukua sampuli za kahawa na kupelekwa makao makuu ya bodi hiyo, Moshi kwenye mashindano yaliyofanyika kwa ushirikiano wa Bodi ya Kahawa Tanzania pamoja na wataalamu waliobobea.

Kufuatia ushindi huo Meneja Mkuu wa WAMACU, Samweli Gisiboye, akizungumza mwishoni mwa wiki aliupongeza uongozi wa bodi chini ya wataalamu wa tathmini kufuatia hatua hiyo na kuahidi kuendelea kulinda nafasi waliyonayo ili kutengeneza mazingira wezeshi kwa wakulima kupata bei iliyo nzuri.

Alisema kuwa chama hicho kilishinda katika shindano hilo lililojumuisha mikoa 16 huku akieleza hiyo ni fursa kwa wakulima watarajie kunufaika hususani katika kupanda kwa bei ya zao hilo sokoni.

Kadhalika, aliwashukuru wakulima na vyama vya msingi na kuwataka kuendelea kuwa mabolozi katika kulinda ubora wa zao hilo ili lizidi kupanda thamani ndani na nje ya nchi.

Ofisa Kilimo Bodi ya Kahawa Mkoa Mara, Rogasian Tarimo, alisema mashindano hayo yanafanyika kila mwaka lengo likiwa kuhamasisha wazalishaji kuongeza ubora wa kahawa, kuzingatia kanuni bora za kilimo na kupata bei nzuri wakati wa mauzo.

"Kwa misimu mitatu ya 2020-2023 taarifa ya Bodi ya Kahawa iliwataarifu wakulima watume sampuli makao makuu Moshi ambapo walianza kuzipeleka Desemba 2022 sampuli 53 zilipokelewa kutoka nchi nzima ambapo uteuzi wa wataalamu wa kutathmini ubora wa kahawa ulianza kwa wataalamu watano walioteuliwa wenye sifa na uzoefu katika ubora wa maswala ya kahawa," alieleza.

Aliendelea kusema kuwa washindi ambao ni WAMACU walipata alama 82.4 na kushika nafasi ya kwanza kitaifa, wakifuatiwa na NYANTIRA AMCOS ambao walipata alama 82.05, wakifuatiwa na Kilimanjaro Plantation ambao walipata alama 82.

Alisema hatua hiyo ni kichocheo cha ongezeko la wanunuzi wa kahawa, kuwataka wakulima kuendelea kulinda ubora huo na kuongeza bidii ya kuzalisha kahawa kwa wingi kutoka tani 354 hadi tani 15,000 ifikapo mwaka 2025 na wanunuzi kupata mzigo wa kutosha na wakulima kunufaika na kilimo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 4, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI





Ukurasa 14

**Wanasayansi wachunguza kasoro zinazoutesa mwili wa binadamu**



Ukurasa 12

Furaha za teknolojia mkaa mbadala kulinda mazingira, kuongeza kipato ilipotua Ilala



Ukurasa 13

Wanafunzi Buhangija Jumuishi walilia walimu elimu maalumu

ELIMU

NA JAMES LAUREAN

# Waandae warithi, kuendeleza vitega uchumi utakapokufa

## •Wafunze kuzitawala fedha, kuthubutu na nidhamu



Mtoto alishe na kutunza wanyama ili afahamu chanzo cha mali hiyo. **PICHA: MTANDAO**

KUMEKUWA na wimbi la malalamiko kutoka kwa wazazi na walezi kuwa wanapata tabu namna ya malezi yakuwapa watoto wao, ili kuwaandaa kurithi na kuendeleza majukumu yao watakapofariki au kuumwa na kushindwa kuendeleza kazi zao.

Ni dhahiri yapo malezi sahihi ya kumpa mtoto kumwandaa na hatima kubwa ya kuendeleza biashara au hata mali na kuiongoza familia kwenye uwekezaji.

Watanzania wanafahamu na wanaona baadhi ya jamii mfano Wazungu, Waarabu na watu wengi wenye asili ya Asia kama China, India wanavyowaandaa watoto wao kuwa warithi wa biashara na miradi ya uwekezaji. Ni juhudi zinazofanywa mapema katika ukuaji wao.

Unaweza kuwakuta watoto wakiuza madukani, au kuwa kwenye maeneo ya uzalishaji katika utoto wao ili kuelewa aina ya biashara.

Katika eneo hilo zipo pia familia zinazowaandaa watoto pengine kwa kuchagua mmoja maalum ambaye hutayarishwa kuwa kiongozi wa biashara, uwekezaji na familia nzima.

Pengine kwa Afrika hakuna juhudi kubwa zinazoonekana hivyo Watanzania wana haja ya kufanya jambo hilo ili kuendeleza na kudumisha mambo bora ya kiuwekezaji na haki za kumiliki na kutunza utajiri wa familia hata baada ya wazazi na walezi kuondoka.

Ethiopia na Somalia kuna jamii zinazofanya jambo hilo, lakini kwa Watanzania utamaduni huo haujafanikiwa na kuacha alama za watu kujifunza, japo kuna baadhi wameweza kuwaachia watoto wao biashara na urithi wa mali.

Nipashe imefuatilia kesi za mirathi mahakamani na kuona kuwa kitu kinachoshtua ni pale walezi wanapokosea katika kupenyeza maarifa, ujuzi wa biashara na usimamizi wa mali hizi kwa watoto ili kuwaanda kuwa warithi wa sasa na miaka ijayo.

Tujiulize ni nini jamii nyingine zinafanya ambazo sisi Watanzania hatufanyi? Kwanini leo kuna biashara kubwa ambazo zinaishi karne nyingi mpaka zimesambaa dunia nzima kutoka kwa mwanzilishi, watoto na sasa ni kwa wajukuu hata vitukuu?

**YAKUZINGATIA**

Kuandaa kizazi chako chenye ushindi kuna vitu unatakiwa uvizingatie tangu wanapoanza kukua na kitaalamu jukumu linaloitwa 'grooming' ambalo linahusisha kile mtoto anachobeba tangu utotoni.

Watu wakumbuke kuwa hata kama utaacha wosia kama hujatengeneza kizazi cha ushindi mali na biashara zipo hatarini. Haziwezi kufika mbali pengine zitakwamia kizazi pili.

**KUTAWALA PESA**

Anaandaliwa kuitawala na kuiheshimu pesa na siyo pesa imtawale au kumzuzua. Katika mambo ambayo jamii ya leo yanamaliza vijana wengi ni kushindwa kuitawala pesa, ni somo ambalo halifundishwi shuleni au chuo chochote.

Inashangaza hata wanaosoma masomo ya biashara wanashindwa kuiweka chini ya miguu yao, hivyo wafundisheni watoto wakiwa na pesa wanapaswa kuzipeleka sehemu gani.

Anatakiwa kununua vitu gani vya faida gani kwake, maamuzi yake anapokuwa na pesa mkononi ni yepi? Anafanya nini na kwa wakati gani?

Katika kumwandaa mtoto mpe pesa na umuone anakimbilia kununua nini, mara nyingi wazazi na walezi wanawapa pesa watoto na wanakimbilia kununua pipi, biskuti, soda na wanataka baiskeli .

Umeshawahi kujiuliza mtoto ukimwelezea kinyume na hayo anaweza kuweka akiba yake mwenyewe, hata kama anahitaji baiskeli? Tengeneza naye bajeti mwambie tunaanza kuweka akiba ya baiskeli ashiriki na aone kuwa yeye anaweza kuitawala pesa.

Kama utashindwa kumfundisha kutawala pesa atafanya ufujaji ataona mali ni nyingi siku atakayoipokea mikononi mwake, atakimbilia kuimaliza na kuishia kufilisika.

VIKAO KUHAKIKI

Suala jingine la kumwandaa mrithi ni kuwa na vikao vya mara kwa mara ukiwa naye kwenye usimamizi wa biashara, mali, kama mashamba, mifugo, ardhi , maduka, hospitali na viwanda au kampuni za huduma.

Mali hailindwi na mikono milegevu, kadhalika biashara hailindwi wala kutunzwana mikono legevu, nguvu unayotumia kuwekeza katika mali zako na utafutaji wako hakikisha nguvu hiyo mtoto anaiona na unamwambukiza

Kama ni shamba unakwenda kukagua mifugo au mazao hakikisha unakwenda naye mara kwa mara aone nini unachofanya, makubaliano unayoingia na wafanyakazi au washirika mbalimbali.

Lakini mzazi au mlezi unapom-

**INAENDELEA UK.12**

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Furaha za teknolojia mkaa mbadala kulinda mazingira, kuongeza kipato ilipotua Ilala

## •Mamia wameibeba, gharama kiduchu faida zaidi

SHIRIKA la Mawasiliano Duniani (ITU), linapoangalia uwepo wa wanawake kwenye nyanja za kiteknolojia linasema kwa mwaka 2019 kunaonekana kuwapo kwa pengo la kijinsia katika matumizi ya mitandao ya simu, kinamama wako chini au hawajahamasika kikamilifu.

Linasema kuna pengo la asilimia 10 na kwamba wanawake ni asilimia 48 na wanaume ni asilimia 58, hivyo kundi hilo kuwa chini zaidi licha ya masuala ya mawasiliano kuanzia simu, televisheni, mitandao ya kijamii kama twitter, whats app, tik tok na you tube.

Hilo ni eneo la mawasiliano, hivyo hata kwenye masuala mengine yanayohusu sayansi na teknolojia wameachwa. Mathalani kutumia teknolojia mbalimbali kutengeneza bidhaa za kujiongezea kipato kadhalika hawaonekani pia.

Ni kutokana na umuhimu wa teknolojia kwa maendeleo ya binadamu kinamama wanashikwa mkono ili wawe washiriki na wasibaki nyuma.

Baadhi ya jitihada zinazochukuliwa ni kuwapa mafunzo ya teknolojia ya kutengeneza vitu mbalimbali, ikiwamo mkaa mbadala unaotumia karatasi mfano, maboksi, majani ya mimea mabichi na makavu na vifuu, yote kwa ajili ya ulinzi wa mazingira lakini pia kujiongezea kipato.

Hivi karibuni wanawake 137 kutoka maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, wanakusanyika pamoja na diwani wa Viti Maalum wa wilaya hiyo, Julieth Banigwa, ili wapate elimu ya kutengeneza mkaa huo muhimu jikoni.



Wanawake wakiwa katika mafunzo ya kutengeneza mkaa mbadala. **PICHA: SABATO KASIKA**

Mwalimu ni Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, Seleman Bishagazi, anayesema hayo juzi, kuwa utawasaidia kuepuka ukatili wa kijinsia kwa vile wana ufahamu na wameongeza kipato.

"Wanawake wananyanyasika katika ndoa kwa sababu hawana kipato, lakini wanaweza kuondokana na ukatili huo, iwapo watakuwa na ujuzi wa kutengeneza mkaa huo mbadala na kuuza lakini wakilinda mazingira na kuepusha ukataji miti ovyo kupata kuni na mkaa," anasema Bishagazi.

Anafafanua kuwa malighafi ya kutengeneza mkaa huo inachomwa pamoja, kisha inamwagiwa maji na kuchanganywa na uji wa muhongo au wa udongo wa mfinyanzi ili kupata umbo lolote la mkaa ambalo mtengenezaji analitaka.

"Mara nyingi nyie wanawake mnadaiwa kuwa ni watu dhaifu, wasio na uwezo wa kufanya mambo makubwa, lakini miaka ya karibuni, mmeibuka kuwa vinara wa kufanya mambo makubwa, kutokana na elimu mnayopewa ya kuwawezesha kujitegemea," anasema.

Anaeleza kuwa kinamama wameendelea kufanya vizuri katika uongozi na hata katika sekta ambayo inatajwa kuwa ngumu, hasa ya sayansi na teknolojia, na kwamba anawatia moyo wazingatie mafunzo hayo.

Mwandaaji wa mafunzo hayo, Julieth Banigwa, anasema amefanya hivyo ili kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, anayewataka viongozi kuzuia ukatili ikiwamo unaosababishwa na umaskini na kukosekana teknolojia.

"Ndiyo maana nikaandaa mafunzo haya yanayoshirikisha wanawake ambao ni viongozi wa Umoja wa Wanawake (UWT) wilaya na wa kata 36 za wilaya ya Ilala wajifunze teknolojia ya kutengeneza mkaa mbadala, ili nao wakawafundishe katika maeneo yao," anasema Julieth.

Anasema matarajio yake katika mafunzo hayo ni kuona wanapunguza migogoro ya ndoa, ukatili wa kijinsia ndani ya jamii, tatizo la ajira, gharama za maisha, uharibifu wa mazingira, kwa kuwa gharama mkaa huo ni ndogo na unatunza miti na uoto wa asili.

"Mkaa wa miti unauzwa Shilingi 2,000 kwa kipimo wakati kipimo cha mkaa mbadala ni Shilingi 1,000, hivyo ni wazi tutapunguza sehemu ya gharama za maisha na kulinda mazingira," anasema Julieth.

Anasema ameandaa mafunzo hayo akitekeleza msemo usemao 'usimpe mtu samaki, mpatie nyavu za kuvulia samaki', kwamba kujifunza teknolojia ya kutengeneza mkaa mbadala ni sawa na kumpa mwanamama vitendea kazi.

Mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo Lydia Kajembe, anasema wanawake wanakabiliwa na vikwazo vingi, kwenye kujikwamua kiuchumi na kwamba mafunzo hayo yameletwa wakati mwafaka.

"Wengi wamekuwa wakiingia katika mikopo ili kufanya biashara na kujikuta katika wakati mgumu ikiwamo ndoa kusambaratika, lakini mafunzo haya yanaweza kuwapunguzi tatizo," anasema Lydia.

Anafafanua kuwa mitaani kuna mikopo mingi ikiwamo iliyopewa majina ya 'kausha damu na roho mkononi' ambayo marejesho yake ni ya kila siku na wanapoyakosa wanachukuliwa mali za familia.

"Unakuta wakati mwingine mwanamke amekopa bila mume kujua, anashindwa kurejesha mkopo, vitu vinachukuliwa, kwa mazingira kama hayo ni lazima kuwe na mgogoro na hatihati."

Lydia ambaye ni Katibu wa UWT Kata ya Segerea, anasema teknolojia waliyopata ya kutengeneza mkaa ataifikisha kwa wengine ili iwasaidie kuondokana na umaskini.

"Kama malighafi ya kutengeneza mkaa huo mbadala ndiyo tuliyoelezwa, maana yake hakuna gharama kubwa ya kukopa fedha kutoka kwa 'kausha damu au roho mkononi ili kuanzisha biashara," anasema.

# WAANDAE WARITHI, KUENDELEZA VITEGA UCHUMI UTAKAPOKUFA

**INATOKA UK.11**

wandaa mtoto hakikisha unamwambia aangalie unachofanya na baada ya hapo ingia naye kwenye maongezi ya nini alichojifunza.

Kama ni biashara unafanya hakikisha unakwenda pamoja naye mwishono mwa wiki na anashiriki, kama mtoto anaweza kuangalia video au katuni na akavutiwa eelewe unachomjengea pia atakishika, unatengeneza kiongozi anayekuja kujua anachofanya hata kama atapata changamoto atakumbuka.

Mfundishe mtoto uaminifu, uthubutu, ujasiri, maadili na walezi na wazazi wengi wanawarudisha nyuma watoto kwa kuwanyima kufanya mambo ambayo wanahisi umri wao bado au wanaona ni kupoteza muda.

Hakuna sababu ya kuwakatisha tamaa watoto wanapoonyesha ubunifu na uthubutu wa aina yoyote wapewe nafasi na uungwaji mkono na kusifiwa kuwa anaweza .

Ikiwezekana shiriki naye katika anachofanya, biashara haitaki kichwa kilicholala inataka moyo wenye uthubutu na akili ambazo utaweza kukupeleka mbele.

Uthubutu ni taarifa kuwa yupo imara kwa utayari kwa mapambano mfundishe kufanya kazi kwa bidii na umfundishe kukataa uvivu, kama mzazi hukutenda kazi kwa mikono milegevu na umepitia mapito mengi mpaka kupata mali na mafanikio ni dhahiri kwamba maisha ya binadamu umefahamu kuwa sio lelemama.

Mikono milegevu huipoteza mali, watoto wafundishwe kufanya kazi na sio tu kazi ni kufanya kwa bidii na kukataa uvivu kabisa katika maisha yao.

Maisha ya vijana wengi tunayaona wanavyotaka vitu rahisi na kugubikwa na uvivu, hivyo lazima watoto wafunzwe kuweka akilini kuwa uvivu ni tatizo na ndicho kinachoangusha maisha ya wengi.

Hilo linafanikiwa kwa kushiriki naye kazi za nyumbani, kumpangia majukumu na kumwamsha mapema kwa mazoezi katika utoto wake.

### NIDHAMU LAZIMA

Wazazi na walezi wafundisheni nidhamu watoto au warithi na kuachilia mbali nidhamu ya pesa fundishe mwanao nidhamu ya kujiheshimu, kumheshimu kila mmoja anayemzunguka na kujali muda, katika biashara nidhamu imebeba asilimia zaidi ya hamsini ya mafanikio.

Mfanyabiashara, mfanyakazi au mwanasiasa anayeshindwa kuwa na nidhamu mafanikio yanakuwa magumu kwake, ni nguzo ya muhimu itakayomfanya ajue namna ya kuwasiliana na jamii katika ngazi mbalimbali.

Mfundishe uvumilivu na ustahimilivu, kama wewe mzazi wakati wa kutafuta mafanikio, fedha na mali ulipitia magumu, basi vivyo hivyo uamini kuwa magumu katika maisha ni sehemu ya nyakati za wote za mafanikio ni hakika pia mwanao atapita nyakati hizi, iwe una pesa nyingi za kutosha au hauna mwandae mwano kisaikolojia azitambue nyakati hizi na aweze kuwa mvumilivu na kustahimili.

Aidha, awe na uwezo wa kufanya maamuzi ya busara katika nyakati kwani ndipo ubora wake utakapoonekana. Tengeneza mazingira ya kumfanya aweze kustahimili mambo madogo nyumbani, mpeleke kwa ndugu kijijini aone mazingira magumu na aishi usimuweke ndani eti hutaki mwanao apate shida.

Wakati mwingine nafasi za Jeshi la Kujenga Taifa JKT zikitoka hakikisha mpambanie aende anachopita huko kinamjenga, anapaswa kuona pande zote za maisha.

### LA MUMIHU

Kundaa mtoto hajjalishi uwe mfanyabiashara mkubwa au mdogo au mfanyakazi ni jukumu la kila mzazi au mlezi katika ngazi yoyote, mfano unaodhihirika wanaofanya hili pia na wanafanikiwa kuwapenyeza watoto wao ni wanasiasa.

Ukiwaangazia wanakupa taswira halisi nini wanafanya kwa wewe ushindwe, tengeneza kizazi chako cha ushindi sasa, linda jasho na mali zako watoto hawatasahau njia na maarifa yako.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Wanafunzi Buhangija Jumuishi walilia walimu elimu maalumu



Baadhi ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule ya Msingi Buhangija Jumuishi Manispaa ya Shinyanga wakiwa darasani. **PICHA: MARCO MADUHU**

WANAFUNZI wenye mahitaji maalumu wanapokuwa kwenye darasa au mazingira ya elimu jumuishi, huwezi kuwatenganisha na hali za maumbile ambayo inahitaji usaidizi wa ziada.

Ndiyo maana upungufu wa walimu kwenye shuleni za umma umekuwa unawapa walimu shida ya namna ya kufundisha na kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Buhangija Jumuishi iliyoko Manispaa ya Shinyanga, Fatuma Jilala, anazungumza na Nipashe kuhusu elimu hiyo, akisema kuwa shule hiyo ina wanafunzi wenye ulemavu 197, wakiwamo viziwi 84, wasioona 30, ulemavu wa viungo wanne, uoni hafifu mmoja na wanaoishi na alibinizu 78 wanaokabiliwa na upungufu wa walimu maalumu.

Anakiri kuwa serikali imekuwa ikiboresha miundombinu ya elimu jumuishi ambazo zinafundisha wanafunzi mchanganyiko wakiwamo wenye ulemavu na wasio na ulemavu, lakini baadhi ya shule hizo zina upungufu wa walimu wenye taaluma maalumu, ikiwamo Buhangija.

"Walimu wanaofundisha viziwi wapo watano, upungufu ni nane na uhitaji ni 19, walimu wasioona wapo wanne upungufu ni mmoja uhitaji ni watano, jumla kuna walimu wenye taaluma maalumu tisa wakati upungufu ni tisa na mahitaji ni walimu 18."

Anasema licha ya kuboresha miundombinu shuleni humo ikiwamo utoaji wa mashine za kuchapisha maandishi ya nukta nundu, kuongeza usikivu, vifaa vya kukuza maandishi kwa wanafunzi wenye uoni hafifu, lakini bila ya kuwapo na walimu maalumu utoaji wa elimu bora utaendelea kuwa changamoto.

Mwalimu Elizabeth Matheo, asiyeona, anasema upungufu wa walimu maalumu shuleni hapo, unawapa wakati mgumu wa kufundisha wanafunzi hao kwa ufanisi.

Anasema uchache wa walimu maalumu umekuwa ukiwafanya kuchoka kufundisha, na kuiomba serikali itatue tatizo hilo la upungufu wa walimu wenye taaluma maalumu shuleni hapo ili kuongeza ufaulu.

> Mwanafunzi mwenye ulemavu Martha Mabula, ambaye anayesoma darasa la sita Buhangija, anasema upungufu wa walimu maalumu ni changamoto kwao kufanya vizuri kitaaluma kutokana na kutofundishwa kwa ufanisi na ufasaha.

Matokeo ya darasa la saba katika shule hiyo jumuishi mwaka jana 2022 ufaulu wa wanafunzi ulikuwa ni asilimia 91, anasema Mwalimu Mkuu Fatuma Jilala na kuongeza kuwa zinafanyika juhudi zaidi kufikia kiwango hicho.

Mwanafunzi mwenye ulemavu Martha Mabula, ambaye anayesoma darasa la sita Buhangija, anasema upungufu wa walimu maalumu ni changamoto kwao kufanya vizuri kitaaluma kutokana na kutofundishwa kwa ufanisi na ufasaha.

Diwani wa Ibinzamata eneo ilipo shule hiyo, Ezekiel Sabo, anasema tatizo hilo la upungufu wa walimu maalumu amekuwa wakilipigia kelele kwenye vikao vya baraza la madiwani na kupewa majibu mepesi kuwa litatuliwa lakini hakuna ambacho kinaendelea.

Ofisa Elimu Taaluma wa Shule za Msingi Manispaa ya Shinyanga Wingwila Kitila, anasema tatizo hilo la upungufu wa walimu maalumu katika shule hiyo linaelekea kupatiwa utatuzi na wanasubiri ajira mpya za walimu maalumu.

Mackrine Shija Ofisa Elimu Kata ya Ibinzamata anasema licha ya shule hiyo kukabiliwa na upungufu wa walimu maalumu, pia wamekuwa wakishirikiana na wadau wa elimu kutoa mafunzo ya elimu jumuishi kwa walimu ili kuongeza ufanisi wa ufundishaji.

"Nawapongeza walimu wa Bugangija licha ya kukabiliwa na upungufu wa walimu maalumu, lakini wamekuwa wakijitahidi kufundisha na matokea yao kitaaluma ni mazuri siyo mabaya," anasema Mackrine.

Mshauri wa Mradi Elimu Jumuishi Dk. Ildephonce Mkama, mradi ambao unashirikisha mashirika manne, Sense International, Tanzania Cheshire Foundation, ADD International na Light For the World, anasema wameshiriki kutoa mafunzo kwa walimu ili kufundisha wanafunzi wenye ulemavu.

Tayari wameshatoa mafunzo ya elimu jumuishi na misingi yake, pamoja na kubainisha watoto wenye ulemavu, ili walimu wawe na uelewa mpana wa kuwafundisha watoto wenye ulemavu na kufanya vizuri kitaaluma.

Kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia tovuti ya Nukta Africa, hadi Februari mwaka huu, kwa nchi nzima kuna upungufu wa walimu maalumu 2,945 kwa shule za msingi jumuishi na waliopo ni 1,517wakati wanahitajika 4,462.

Elimu jumuishi inaelezwa kuwa ni njia bora ya kuwa na jamii jumuishi na shirikishi licha ya kwamba kuna vikwazo ambavyo vinapaswa kueleweka na kutambuliwa ili viweze kuondolewa kwa lengo la kupata ufanisi.

Mathalani, shule kutokuwa na miundombinu ya kutosha au wakati mwingine haina huduma hizo ambazo zingewawezesha wanafunzi wenye ulemavu kujumuika na wenzao na kujifunza.

Elimu jumuishi siyo tu kuwaweka pamoja watoto wenye ulemavu kwenye shule za kawaida na kuacha wao wenyewe kujituma na kujiongeza ili kumudu masomo na skili mbalimbali wanazofundishwa inahusisha pia kuweka mifumo ambayo inawezesha watoto hao kumudu na kushindana kimasomo na skili nyingine na wenzao, aidha, kuwa na mbinu za ufundishaji za kuwawezesha kujifunza na waweze kujifunza kwa ukamilifu kama wenzao bila kuona usumbufu.

Lengo la elimu hiyo ni kuwawezesha watoto washirikiane kwa kina kwenye kila jambo na kuwafanikisha kuishi maisha yenye utu, wanayojenga ndoto zao na waweze kufikia kwa mustakabali wao wenyewe badala ya kutengwa na kuonekana kuwa wana mahitaji na mkondo maalumu kielimu mbali na ule unaotumika kwenye jamii nzima.

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Wanasayansi wachunguza kasoro zinazoutesa mwili wa binadamu



Viungo vya wanyama jamii ya vyura na nyoka vya uzazi vinaelezwa kufichwa kwa usalama zaidi kuliko vya binadamu.

WANASAYANSI wanaochunguza mwili wa binadamu wanasema wamegundua una upungufu mwingi na katika utafiti mbalimbali wameona hayo.

BBC inasema hayo yanagundulika baada ya mageuzi mengi ya mwili huo, kasoro kadhaa zilizobakia katika mwili wa mwanadamu zinadhihirika.

Inazitaja kuwa baadhi ya hitilafu hizo kati ya nyingi ni pamoja na mfano wa kwenye muundo wa uzazi wa wanaume au wa kiume, sayansi ikipendekeza kuwa ingekuwa vyema kama kiungo chake cha uzazi kingelindwa kama mapafu, moyo au ini tena kisiachwe kuwa wazi.

Hivyo kingefichwa na kisionekane ili tu wakati wa kujamiiana pekee na baada ya hapo kiishi mafichoni.

Wanaamini kuwa kiungo au sehemu hiyo ya siri kuwa nje kama ilivyo sasa kunaleta tatizo kwenye mbegu za kiume kwamba haziwezi kukua vizuri kwa joto la kawaida la mwili, yaani nyuzi joto 36.5 hadi 37 sentigredi.

Wanasayansi wanatoa mfano wa wanyama wengine, hasa wale ambao hawana damu joto au wenye damu baridi kama vyura, viungo vyao vya uzazi vya kiume vinalindwa vyema na vimefichwa kwa ndani.

Hata wanyama wengine wenye damu joto, kama vile tembo, wana viungo vya uzazi ambavyo ni salama zaidi siyo kama vya wanadamu wakiume.

Wanaamini kuwa sehemu hiyo kuachwa kama ilivyo kumekuwa na upungufu kwenye kustawi vizuri kwa mbegu za kiume na huenda kunachangia shida nyingi zinazoibuka kutokana na hali wanayoiona kwenye mfumo huo.

**UTI WA MGONGO**

Uti wa mgongo una maumivu ambayo wataalamu wanahisi chanzo chake ni tatizo la jinsi ulivyoumbwa.

"Bila shaka mfano mwingine wa jinsi mwili wa mwanadamu ulivyo na kasoro kisayansi ni 'mgongo'" inasema BBC.

Je, unaweza kupata mtu ambaye hajawahi kukutana na tatizo au kuumwa mgongo katika maisha yake?

Inaongeza kuwa mifupa ya mgongo hukaa kwa utaratibu ambao ni kama kuunda upinde unaoshikilia vyema muundo wote wa mwili wa mnyama pamoja akiwamo binadamu.



Bibi kizee aliyepinda mgongo kutokana na hitilifu wanazoziita ni kasoro. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Lakini kwa kuwa binadamu ni aina ya mnyama mwenye miguu miwili, pingili za mgongo zimepangwa kiuhalisi katika safu za 'longitudinal', ikimaanisha kuwa zimelala kuanzia juu hadi chini kwa utaratibu ambao unamletea kuumwa.

Kutokana na aina hii ya mpangilio, BBC inaeleza kuwa wanasayansi wanaona kuwa pingili katika sehemu ya chini ya mwili 'vertebrae' inapaswa kubeba uzito zaidi wa mwili.

Ndicho chanzo cha tatizo la maumivu ya kiuno na mgongo kwa binadamu ambalo sasa linaonekana kuwa ni la kawaida.

**UPOFU MACHONI**

Jicho la mwanadamu pia wanasayansi wanalitaja kuwa ni udhihirisho wa mfano wa udhaifu wa mwili wa kiumbe huyo.

Retina ya binadamu imefunikwa na jukumu au kazi ya retina ni kunasa au kupokea taarifa nyepesi na kutuma taarifa hizo kwenye ubongo kupitia mshipa wa macho.

Shida inayoonekana ni kwamba hakuna vipokezi vya picha katika hatua ambapo neva ya macho huvuka retina, hii inamaanisha kuwa binadami wana 'sehemu isiyoonekana' au 'upofu' katika kila jicho.

Wanyama wengine hawana madoa machoni kama walivyo watu kwa mfano samaki pweza.

Katika macho ya pweza, nyuzinyuzi za macho ziko nyuma ya retina, hivyo neva ya macho haihitajiki kupeleka taarifa nyepesi kwenye ubongo ili kutambua na kung'amua alichoona.

Kwa sababu hii, hakuna kikwazo au kizuizi machoni pa pweza kama ilivyo kwa binadamu, hivyo haathiriki na upofu wala kutoona.

**KOO/ KUKOHOA**

Ukosefu wa hewa ni sababu kuu ya kifo kisicho cha kawaida miongoni mwa wanyama wenye afya, mathalani waliokufa kutokana na kukosa hewa ilikuwa mara mbili zaidi ya idadi ya watu waliopoteza maisha kwa ajali za magari huko nchini Hispania.

Mirija ambayo hubeba chakula na hewa katika miili imeunganishwa kwa namna hatari katika sehemu kadhaa za mwili.

'Pharynx' ni kiungo muhimu ambacho ni kama bomba ambalo huanzia puani kwa ndani kwenda chini ya shingo na kooni.

Kwa kawaida, maji na chakula vinakwenda kwenye kitu kinaitwa 'esophagus' au koo wakati hewa inakwenda ama kupitia kwenye 'trachea' au koromeo.

Lakini kuna wakati mwingine mambo yanaweza kwenda vibaya katika mfumo huo, BBC inatahadharisha kwamba ikiwa hata kiasi kidogo cha chakula kinaingia kwenye 'trachea' au koromeo la hewa kwa bahati mbaya wakati wa kula, inaweza kusababisha madhara makubwa kama vile kifo kwa kukosa hewa.

Na hii inathibitisha kwamba mfano binadamu hawezi kula kwa haraka kwa sababu mwili wake haujaundwa kuruhusu hali hiyo, wanasayansi wanasema.

**LA MUHIMU**

Wanasayansi wanasema kuwa yapo mapungufu mengi ya kimwili na kimfumo ambayo ni utafiti na uchunguzi unaofanyika katika kujifunza na kuufahamu zaidi mwili pengine kwa minajili ya tiba na hasa kulinda maisha.

Wanasema ni maoni ambayo hayaingiliani na imani wala ma makala haina ni wala sababu ya kukosoa uumbaji, kutokana na imani za wanadamu, bali kuonyesha dhana ya kisayansi katika mwili wa mwanadamu baada ya kuuchunguza na kutafuta vyanzo vya maradhi.



## Uwanja wa Mashujaa kuwa wa viwango vya kimataifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, amesema ujenzi wa Uwanja wa Mashujaa, katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma utakapokamilika utakuwa wa viwango vya juu na mfano barani Afrika.

Mhagama aliyasema hayo jana alipokuwa akikabidhi kipande cha sehemu ya ujenzi ya uwanja huo unaotekelezwa na kampuni ya SUMA JKT baada ya kukamilika kwa sehemu ya kwanza ya ujenzi wa uwanja wa gwaride ambao unategemewa kutumika kwenye maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa Julai 25, 2023.

"Eneo hili ni sehemu ya kwanza ya ujenzi wa eneo la maadhimisho ya Uwanja wa Mashujaa, (Parade Ground) ambayo itakuwa na mnara wa mashujaa wenye ubora na viwango vya juu kabisa," alisema.

Alifafanua kuwa awamu ya pili itakuwa na bustani kubwa, ambayo itakuwa na mvuto wa aina yake na tayari taasisi mbalimbali za serikali zimeonesha nia ya kuwekeza na kushirikiana kuhakikisha kutakuwa na bustani hiyo yenye migahawa, viwanja vya michezo na burudani.

Waziri huyo alisema sehemu ya tatu itahusisha ujenzi wa mnara mrefu wa zaidi mita 110 ambao utakuwa mnara wa kwanza barani Afrika ambao utakuwa ni kivutio kwa watalii na kuongeza pato la taifa.

Alisisitiza serikali pamoja na kuhamia Dodoma imejenga miundombinu yenye hadhi ya makao makuu ya serikali na jamii inashuhudia majengo ya serikali makubwa na miundombinu mingine ikiendelea kukamilishwa.

Naye Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Dk. Jim Yonazi, alisema uwanja huo utakapokamilika utaongeza uzuri na ubora wa Jiji la Dodoma na serikali itahakikisha kwamba mnara pamoja na uwanja wake unakuwa wa kupendeza na kuwa na mvuto wa kipekee.

Awali akizungumza katika makabidhiano hayo, katibu wa kikosi kazi cha taifa cha kuratibu serikali kuhamia Dodoma, Meshack Bandawe, alisema ujenzi huo umezingatia suala la mpango kabambe wa ujenzi wa mji wa serikali na kazi ya ubunifu wa awali ilifanywa kwa kina na wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, Mamlaka ya Bandari (TPA), Shirika la Nyumba (NHC) na SUMA JKT.

Mwakilishi wa kampuni ya ujenzi kutoka SUMA JKT Kanda ya Kati, Meja Samweli Jambo, alisema ujenzi huo umefuata taratibu zote za upimaji na viwango.

Alisema: "Tulifanya kazi usiku na mchana kuhakikicha tunatekeleza maelekezo ya waziri ya kukabidhi kipande hiki kwa wakati".

# Dk. Nchemba ahimiza matumizi Sensa ya Watu na Makazi 2022

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amewataka watendaji wa serikali kuzingatia matumizi sahihi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka jana katika kupanga mipango ya maendeleo.

Dk.Nchemba alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akifunga mafunzo ya usambazaji na matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa viongozi wa Mkoa wa Singida na wilaya zake yaliyofanyika wilayani hapa.

Alisema mipango mingi inashindwa kutoa huduma kwa wananchi kutokana na kutokutumia takwimu za Sensa ya Watu na Makazi zilizopo katika kupanga mipango hiyo.

Nchemba alisema viongozi wa serikali na wananchi kuanzia sasa wahakikishe wanazitumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi katika mipango ya maendeleo ili kuepuka changamoto zinazojitokeza pale ambapo takwimu sahihi hazijatumika.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema mipango ya maendeleo ya Mkoa wa Singida itazingatia matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi.

Serukamba alisema ili wananchi wa Mkoa wa Singida waweze kupata huduma bora na mipango ya mkoa, serikali itazingatia matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Mtakwimu Mwandamizi, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Mdoka Omary, alisema malengo ya mafunzo hayo kwa viongozi wa Mkoa wa Singida na halmashauri zake ni kuwajengea uwezo wa kutumia takwimu katika kupanga mipango ya maendeleo katika maeneo yao.



Ofisa Itifaki Mkuu kutoka Kitengo cha Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa Ofisi ya Waziri, Pascal Mageka, akitoa maelezo namna ya matumizi ya eneo litakavyotumika wakati wa gwaride. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanufaika BBT watakiwa kuhamasisha wenzao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, amewaasa vijana waliopata fursa katika programu ya BBT kuhamasisha wengine kushiriki kwenye kilimo ili kujikwamua kiuchumi.

Mavunde alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akikagua maendeleo ya vijana wanaopata mafunzo kupitia programu hiyo kwenye Kituo cha Bihawana mkoani Dodoma.

Aliwataka vijana hao kutumia fursa hiyo waliyoipata kuchochea na kuleta mageuzi kwenye sekta ya kilimo.

"Muwashawishi vijana wengi zaidi kushiriki kwenye sekta ya kilimo ili kundi hili kubwa la vijana litoe mchango kwenye kukuza sekta ya kilimo nchini na serikali itaendelea kuhakikisha inaboresha mafunzo haya ili kuwaandaa vyema vijana katika utekelezjai wa malengo ya ajenda 10/30," alisema.

Naye mratibu wa programu ya BBT, Vumilia Zinkankuba, alisema programu hiyo inaendelea katika vituo 13 kwenye maeneo mbalimbali nchini na sasa ipo hatua za mwisho za mafunzo ya darasani na shambani.

Alisema baada ya kukamilika hatua hiyo vijana hao watapelekwa shambani kuanza uzalishaji wa mazao kwa vitendo.

Kiongozi wa vijana hao, Razack Mbaraka, alisema programu hiyo imekuwa na mchango mkubwa katika kuwaongezea maarifa juu ya kilimo biashara na hivyo kuwaandaa kuja kushiriki kikamilifu kwenye sekta hiyo.

"Tunamshuruku Rais Samia Suluhu Hassan na Wizara ya Kilimo chini ya uongozi wa Hussen Bashe kwa fursa hii ya mafunzo ya kilimo na kumilikishwa ardhi kwa vijana kupitia programu hii ya BBT."

Alisema: "Tangu tumejiunga hapa tumejifunza mambo mengi na kuongeza ujuzi mkubwa kwenye eneo la kilimo biashara, ni ahadi yetu kwamba kupitia mafunzo haya tutasaidia kuchochea ukuaji wa sekta ya kilimo kwa kulima kitaalamu na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo."





# Miradi ya barabara Mbeya yakamilika kwa asilimia 95

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MIRADI ya ujenzi wa barabara katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya ambayo ilitengewa fedha katika bajeti ya serikali iliyomalizika imekamilika kwa zaidi ya asilimia 95.

Aidha, miradi ambayo ujenzi wake inaendelea inatarajiwa kukamilika Septemba mwaka huu kulingana na mikataba ya makandarasi waliopewa tenda.

Miradi hiyo ni ile inayosimamiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Meneja wa TARURA Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Wilson Charles, alisema halmashauri hiyo ilitengewa zaidi ya Sh. bilioni tano ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa barabara pamoja na matengenezo.

Alisema baadhi ya barabara hizo zimeshakamilika na zingine ziko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji kulingana na mikataba yake na kwamba mikataba yote inakamilika Septemba.

Alisema barabara hizo zinajengwa kwa kutumia fedha zinazotokana na vyanzo mbalimbali ikiwamo fedha kutoka serikalini na zingine kutoka kwa wadau.

"Mwaka huu wa fedha tuna mipango mingi ikiwamo ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 10 ambazo tutazijenga kwa kiwango cha lami na hizi ni barabara zinazosimamiwa na TARURA," alisema Mhandisi Charles.

Alisema malengo waliyonayo ni kwamba mpaka kufikia Julai 2024 Jiji la Mbeya litakuwa na barabara mpya zilizojengwa kwa kiwango la lami zenye urefu wa zaidi ya Km. 30 pamoja na miundombinu mingine muhimu ikiwamo mitaro.

Baadhi ya makandarasi wanaotekeleza miradi hiyo ya ujenzi wa barabara katika Jiji la Mbeya walisema watahakikisha wanakamilisha miradi hiyo ndani ya muda uliopangwa kwenye mikataba yao.

Mmoja wa makandarasi hao, Nkala Mussa, alisema wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo walikuwa wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo uhaba wa malighafi za ujenzi lakini hiyo haikuwakwamisha.

Alisema walikuwa wanapata malighafi ambazo baadhi zilikuwa hazikidhi vigezo lakini baada ya kuzipata wanaendelea na utekelezaji wa miradi hiyo.

Alisema wamekuwa wakipata ushirikiano kutoka serikalini na kwa wadau mbalimbali wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo jambo ambalo limekuwa likiwasaidia kutekeleza bila kukwama.

"Kwa kasi tuliyonayo sasa hivi ni kwamba tuna uhakika miezi miwili iliyobakia tutahakikisha tunamaliza miradi hii, kwa sasa hatuna kikwazo cha aina yoyote, vifaa tunavipata ni vile vinavyokidhi vigezo," alisema Nkala.

Baadhi ya wananchi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya walisema miundombinu inayojengwa kwenye maeneo yao ina faida kwao kutokana na kurahisisha shughuli zao za usafiri na usafirishaji.

Mmoja wa wananchi hao, Daud Kamwela alisema baadhi ya barabara hizo zitasaidia kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara kuu.

Alisema mwingiliano wa bajaji na magari ya abiria ambao umekuwa ukisababisha migomo ya mara kwa mara ya magari hayo itafikia mwisho.



Diwani wa Viti Maalum, Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, Julieth Banigwa, akizungumza mwishoni mwa wiki katika mafunzo ya ujasiriamali aliyoandaa kwa ajili ya Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) wa wilaya hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TARI-Uyole yagundua mbegu ya kisasa ya mafuta

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UHABA wa mafuta ya kupikia uliolikumba taifa kwa miaka miwili iliyopita umeanza kupatiwa ufumbuzi baada ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya kugundua mbegu za kisasa zenye mafuta mengi.

Mbegu hizo zijulikanazo kwa jina la 'rekodi' tayari zimeanza kusambazwa kwa wakulima na inaelezwa kuwa zikizalishwa kwa kufuata mbinu bora za kilimo nchi itaondokana na tatizo la upungufu wa mafuta.

Mtafiti wa mazao ya mafuta kutoka TARI kituo cha Uyole, Beatha Paulo, alisema matumizi ya mbegu duni za mazao yanayozalisha mafuta ya kupikia nchini kama vile alizeti ndio ambao ulisababisha uhaba wa mafuta ya kupikia nchini. Alisema kwa sasa tatizo hilo tayari wamelipatia ufumbuzi kwa kugundua mbegu bora za alizeti ambazo zimeanza kusambazwa kwa wakulima.

Alisema kwa sasa taasisi hiyo imewezeshwa na serikali kuzalisha mbegu nyingi ambazo zinatosheleza mahitaji ya wakulima katika maeneo yote yanayozalisha zao hilo nchini.

"Wakulima wengi wamekuwa wakitumia mbegu za kienyeji ambazo hata uwezo wake wa kuzalisha mafuta ni mdogo, kwahiyo sasa hivi tunawakaribisha kuja kuchukua mbegu hapa ambazo tumezifanyia maboresho," alisema Betha.

Aliwataka Watanzania kuachana na kilimo cha kienyeji cha kutumia mbegu za kienyeji na badala yake watumie mbegu za kisasa ambazo zimefanyiwa utafiti na kufuata mbinu bora za kilimo.

Hata hivyo baadhi ya watafiti wa taasisi hiyo, waliomba serikali kusaidia kuimarisha shughuli za utafiti na kuwezesha usambazaji wa teknolojia mpya zinazogunduliwa ili ziwafikie wakulima katika maeneo mbalimbali.

Mtafiti kutoka katika Kitengo cha Uhawilishaji wa Teknolojia na Uhusiano wa TARI Uyole, Rehema Chiumbe alisema wanazalisha teknolojia mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha shughuli za kilimo.

Alisema ili kuhakikisha teknolojia hizo zinawafikia wananchi wanatumia mbinu mbalimbali kuhakikisha zinawafikia ikiwemo maonyesho, vyombo vya habari pamoja na kuwatembelea wakulima kwenye maeneo yao.

Aliiomba serikali kuwasaidia ili kuhakikisha wanawafikishia wakulima teknolojia hizo bila kikwazo cha aina yoyote hasa vinavyohusiana na masuala ya uchumi.

"Tunawaalika wakulima kutoka maeneo mbalimbali nchini kuja kujifunza teknolojia tulizonazo hapa, hizi mbegu za alizeti tunazozalisha ni bora na zimefanyiwa utafiti lakini haitoshi kuzalisha lazima tuzisambaze kwa wakulima," alisema Rehema.

Alisema lengo la taasisi hiyo ni kusaidiana na serikali kumaliza tatizo la uagizaji wa mafuta ya kupikia kutoka nje ya nchi jambo ambalo alisema linaigharimu serikali fedha nyingi.

Nao baadhi ya wakulima waliopewa mbegu hizo kwa ajili ya kuzilima kwa majaribio walisema mbegu hizo zina tija kuliko za asili ambazo walikuwa wanazitumia siku zote.

Mmoja wa wakulima hao, Alinanuswe Mwakilasa, aliishukuru serikali kwa kuwapatia mbegu hizo kwa maelezo kuwa zitawasaidia kujiinua kiuchumi.

Alisema mbegu za kienyeji ambazo walikuwa wanazitumia muda mrefu zina mafuta kidogo ikilinganishwa na za kisasa ambazo wamepatiwa na TARI.

## RC ataka kasi zaidi ujenzi hospitali ya wilaya

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, imetakiwa kusimamia mradi wa upanuzi wa hospitali ya wilaya hiyo na kuhakikisha unakamilika mapema ili wananchi waendelee kupata huduma.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipoweka jiwe la msingi la upanuzi wa hospitali hiyo ambapo Serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya upanuzi na ununuzi wa baadhi ya vifaa.

Alisema majengo yanayojengwa kwenye hospitali hiyo likiwamo jengo la wajawazito yanatakiwa kujengwa kwa viwango vinavyokusudiwa na serikali ili thamani halisi ya fedha ionekane.

Alisema baada ya muda huo kuisha atakwenda katika wilaya hiyo kwa ajili ya kuyazindua majengo hayo ili yaendelee kufanya kazi ya kuwahudumia wananchi.

Alisema serikali iliamua kuipanua hospitali hiyo ili kusogeza huduma mbalimbali kwa wananchi wa wilaya hiyo na kupunguza msongamano kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya na Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

"Lakini hapa kuna jengo ambalo linajengwa na wenzetu UNICEF (Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto), waambieni wajaribu kuongeza kasi ili nalo likamilike haraka na lianze kutoa huduma kwa wananchi," alisema Homera.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inaimarisha huduma za afya kwa wananchi kwa kuhakikisha inajenga zahanati katika kila kijiji, kituo cha afya katika kila kata na hospitali ya wilaya kwenye kila wilaya ili wananchi wasitumie muda mrefu kutafuta huduma hiyo.

Alisema hospitali ya wilaya inatakiwa itumike kama rufani kwa wagonjwa ambao wanashindwa kuhudumiwa kwenye zahanati na vituo vya afya.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, aliahidi kusimamia kwa weledi utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike kwa wakati kama ambavyo walielekezwa na kwamba watahakikisha ubora wa mradi huo unakuwa kama ambavyo serikali inakusudia.





# ZRA yakusanya bil.565/- mwaka wa fedha 2022/23

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Zanzibar (ZRA) imefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 565.8 katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 sawa na ufanisi wa asilimia 97.65 kati ya Sh. bilioni 579 walizopangiwa kukusanya.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Kamishna wa mamlaka hiyo, Yusuphu Juma Mwenda, alisema ukusanyaji huo wa mapato ni ufanisi mkubwa ikilinganishwa na mwaka 2021/2022 ambao walikusanya Sh. bilioni 374.295.

"Kwa hiyo ukifananisha na tulizokusanya mwaka huu wa 2022/2023 Sh. bilioni 565.5 tumekuwa kwa asilimia 51.19 inamaana tumekusanya zaidi ya mara moja na nusu tulichokusanya mwaka 2021/2022," alisema Mwenda.

Kamishna huyo alisema sababu zilizochangia kukusanya makusanyo mengi ya kodi ni ukuaji wa uchumi ambapo shughuli nyingi za kiuchumi zimeongezeka, kuboreshwa huduma za ZRA kwa walipa kodi ikiwamo mifumo ya utoaji wa risiti za kielektroniki na mfumo wa usimamizi wa kodi za ndani.

Alisema mfumo huo wa usimamizi wa kodi za ndani umeanza na walipakodi wakubwa na wameshasajiliwa na katika kipindi cha Julai hadi Septemba watahakikisha walipa kodi wa kati na wadogo wanasajiliwa.

Aidha, alisema mfumo huo pia unawezesha kuunganisha na mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hivyo itarahisihsa biashara za Zanzibar na Tanzania Bara na kuunganisha na mifumo ya Bandari ili kujua nani anaingiza kipi na anatakiwa kulipa vipi.

"Pia tutaunganisha na mifumo ya wafanyabiashara wakiwamo wenye hoteli, maduka makubwa na wenye biashara zingine kwa hivyo tumeanza,umetusaidiakiasinakwa sasa tutaimarisha zaidi," alisema.

Alitaja sababu nyingine ni kuimarika kwa ufanisi ndani ya ZRA ambayo imesaidia kuongezeka kwa asilimia 51 ya mapato, kuongeza walipa kodi ambapo wamefanikiwa kusajili walipa kodi wapya 5,504 na kufanya kaguzi ili kubaini wasiolipa kodi.

Alisema hatua hiyo imesaidia kuongeza ulipaji kodi lakini pia kukusanya madeni na kufuatilia mrejesho kwa wakati na kuwapongeza wafanyabiashara wanaowajibika katika ulipaji wa kodi.

Mwenda alisema mikakati ya mwaka mpya wa fedha wa mwaka 2023/2024 ni kukusanya kodi, kutoa huduma bora zaidi kwa walipa kodi, kutoa elimu ya kodi ili kukusanya kodi ya serikali kwa maendeleo ya Zanzibar.

Alisema utalii unachangia zaidi ya asilimia 30 ya ukusanyaji wa kodi, hivyo lazima kuboresha mazingira ya miundombinu na ni vyema wageni kuchangia kodi ya miundombinu ambayo mgeni akilala katika hoteli yenye hadhi ya nyota tano kuchangia Dola tano ya Marekani.

Akizungumzia changamoto ambazo zimekwaza ufanisi wa ukusanyaji wa kodi katika mwaka wa fedha ulioisha alisema bado ulipaji wa kodi wa hiari upo chini, elimu ndogo ya ulipaji wa kodi kwa wananchi na wapo baadhi ya wafanyabiashara wachache wanakwepa kulipa kodi.

Mwaka wa fedha 2023/2024 ZRA imepangiwa kukusanya Sh. bilioni 675.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Yusuph Juma Mwenda, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari ofisini kwake Mazizini kuhusu makusanyo ya kodi kwa mwaka 2022/2023. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tamasha usomaji vitabu kuanza rasmi Oktoba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale kwa kushirikiana na Jumuiya ya Fasihi Zanzibar imepanga kufanya tamasha la usomaji wa vitabu Zanzibar Oktoba mwaka huu.

Waziri wa wizara hiyo, Simai Mohammed Saidi, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari akisema tamasha hilo litakuwa la kwanza kihistoria la kibiashara la kimataifa la vitabu kufanyika visiwani humo.

Alisema tamasha hilo linatarajiwa kuwa la siku tatu ambalo litatangazwa kitaifa, kikanda na kimataifa na linaendana na dhana ya utalii, mikutano na matukio.

Alisema kuwa tamasha hilo litawashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wanafunzi, wasoma vitabu, wanataaluma, wakurugenzi wa taasisi za elimu, wafanyabiashara wa vitabu, wachapishaji na wakuu wa taasisi za kitamaduni pamoja na wananchi wa Zanzibar.

Alisema matamasha hayo yatawajumuisha wanafunzi kwenye fani ya mitindo na kuwakutanisha pamoja ili lengo la kubadilishana mawazo na kujifunza kutoka kwa wabobezi wakongwe.

Wakati huo huo, Waziri Simai, alitangaza kamati ambayo itasimamia tamasha hilo ambao ni Dk. Maryam Jaffa, Ali Baharoon, Zainab Alwi Baharoon, Kawthar Buwayhud, Ali Saldh, Abdallah Khamis Ali, Profesa, Abdul Sharif, Dk. Abdulla Mohamed Juma na Ali Amour.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Fasihi, Ali Baharoun, alisema katika njia ya kuanzisha tamasha hilo kutasaidia waandishi kutambulika duniani pamoja na kuongeza pato la taifa.

# Serikali yawakaribisha wadau katika utunzaji mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema serikali ipo tayari kufanya kazi na washirika wa maendeleo pamoja na wataalamu tofauti katika kuendeleza jitihada za utunzaji wa mazingira ikiwamo ya baharini.

Aliyasema hayo jana alipofanya mazungumzo na ujumbe wa Taasisi ya NOAH's ARK kutoka Afrika Kusini wanaojishughulisha na utunzaji wa viumbe wa baharini.

Ujumbe huo umefika Zanzibar kuonana na viongozi wakuu, kuwasilisha wazo la mradi huo wa utunzaji wa mazingira ya Bahari, kwamba wanakusudia kujenga mabwawa maalumu katika maeneo mbalimbali baharini visiwani humo kwa ajili ya kutunza viumbe hai wa baharini.

Makamu huyo alisema kwamba serikali inapokea wazo la kuwapo mradi huo na kuwaeleza wawekezaji hao kwamba ipo tayari kutoa ushirikiano unaohitajika katika ngazi za kisiasa na utaalamu ili muda utakapowadia mradi huo uweze kutekelezwa kwa ufanisi na kusaidia suala la utunzaji wa mazingira Zanzibar.

Alisema kwamba serikali inafurahia wazo la mradi huo kuletwa Zanzibar na kwamba kupitia ngazi mbalimbali za watendaji ipo tayari kuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi huo ambao utachangia jitihada za nchi katika kupambana na tatizo la uharibifu wa mazingira.

Hata hivyo, Othman alisema kuna haja ya wananchi kupatiwa elimu ili kuwa na upeo na ulewa wa kutosha kuhusu suala la uwepo mradi huo ambao ni muhimu katika jitihada za kunusuru mazingira ya Zanzibar.

Aidha, alisema kufanya hivyo kutasaidia kurahisisha kwa wepesi utekelezaji wa mradi huo muda utakapowadia na hivyo kuchangia kupatikana ufanisi bora na kutimiza malengo ya mradi huo.

Aliwataka viongozi wa taasisi hiyo kukutana na wataalamu wa Zanzibar ili kufanya mashauriano ya kisera na kitaalamu na kusaidia fikra na kuwapo maamuzi sahihi ya kuandaa mradi huo.

Mtendaji Mkuu wa taasisi hiyo, Kanda ya Afrika, Richard Curson, alisema wameichagua Zanzibar kuanzisha mradi huo baada ya kupata ridhaa na baraka za serikali, kwamba wanakusudia kutengeneza mabwawa ya kuhifadhia viumbe wa baharini katika maeneo mbalimbali.

Aidha, alisema utekelezaji wa mradi huo pia itakuwa ni kichocheo kikubwa cha kuimarisha sekta ya utalii jambo litakalochangia upatikanaji na uimarishaji wa suala la ajira kwa vijana wa Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT.**
**(CAP. 117 R.E 2002)**
**DEED POLL/CHANGE OF NAME**

THIS CHANGE OF NAME DEED is made this 21st day of OCTOBER 2019 by me FARIDA MALAU MBWANA formerly known as FARIDA MALLAN MBWANA of P.O. Box..........Dar es salaam.

WITNESSES AND IT IS HEREBY DECLARED as follows:

- I absolutely renounce and abandon the use of my said former name of FARIDA MALLAN MBWANA and I assume and determine to take substitution of my former name of FARIDA MALLAN MBWANA.
- AND IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid I DECLARE that I shall, at all times hereafter, in all records, documents and other writings and in all actions and dealings and on all occasions whatsoever use the new name of FARIDA MALAU MBWANA in substitution for my former name of FARIDA MALLAN MBWANA.
- So relinquished as aforesaid to the intent that I may hereafter be known not by the aforesaid former name, but by the new name of FARIDA MALAU MBWANA.
- AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE all persons at all times to designate, describe and address the new name of FARIDA MALAU MBWANA.

IN WITNESS WHEREOF I have hereunto subscribe my new name of FARIDA MALAU MBWANA and have affixed my signature the day and year herein written.

SIGNED and DELIVERED by the said FARIDA MALAU MBWANA who is known to me personally/identified to me by the latter known to me personally in my presence This ....21.... day of ....10.... 2019 } DEPONENT

BEFORE ME:
NAME: TEDDY M. CHARLES
ADDRESS: P.O BOX 11587 DAR ES SALAAM
SIGNATURE:
QUALIFICATION: COMMISSIONER FOR OATHS



---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU MTWARA**
**SHAURI LA MAOMBI YA JINAI NA. 6/2023**
**(Asilia shauri la jinai Na. 18/2021, Mahakama ya wilaya Liwale iliyopo Wilaya ya liwale)**
**MKURUGENZI WA MASHTAKA............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**RAJABU MOHAMED NGATANDA NA WENZAKE............ WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA**

1. RAJABU MOHAMED NGATANDA
2. OMARI BAKARI HOKORORO
3. HUSSEIN ABDALLAH NGUDU
4. MOHAMED ABDALLAH SALUM
5. HAJI RASHID LIKWAWATU
6. AHMAD SALUM MPOTO

**POPOTE MLIPO TANZANIA**

HII NI KUWATAARIFU KUWA MNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUSIKILIZA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 10/7/2023 SAA 2:30 ASUBUHI BILA KUKOSA.

KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA, BASI SHAURI HILI LITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO.

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 7/06/2023

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MWACHIA YAYAHA ALLY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA PREMIO yenye jina la umiliki MINGOYO SAWMILL CO. LTD yenye usajili namba T 764 BAK , CHASSIS NAMBA: ATA2110107444 na ENGINE NAMBA: 7AH526495. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**DAR/MSI/RB/222537/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 94 YA 2023**
**(Yanayotokana na Maombi No 245/2021)**

**TABU JOHN............................................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**FRANK AVERINE MBOWE........................MJIBU MAOMBI**
**FINCA MICROFINANCE BANK................MJIBU MAOMBI**
**BOSTON AUCTION MART AND GENERAL AGENCY CO LTD ...........MJIBU MAOMBI**
**TUJIJENGE TANZANIA LTD....................MJIBU MAOMBI**
**NMB BANK...................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA: FRANK AVERINE MBOWE BOSTON AUCTION MART AND GENERAL AGENCY CO LTD**

Popote mlipo mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro tarehe **19/07/2023** mbele ya Mwenyekiti E. Mogasa ninyi wenyewe binafsi au mtume mwakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yanu na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa **MKONO** wangu na **MUHURI** wa Baraza leo tarehe **30, mwezi Juni, 2023**

E.MOGASA
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO

---

**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**
**AT KINYEREZI**
**CIVIL CASE NO.2/2023**
**HAMZA SAID MOHAMED ...............PLAINTIFF**
**VERSUS**
**MICRO ENSURE TANZANIA LTD............DEFENDANT**
**TO MICRO ENSURE TANZANIA LTD**
**P.O.BOX 38605**
**DAR ES SALAAM**

**TAKE NOTICE** that the plaintiff has instituted a suit against you with particulars of claim set out in a plaint filed in this court.

Service of the summons on you has been ordered by means of this publication. You are difected to collect copies of the summons and plaint from the court's Registry.

You are hereby summoned to appear in this court in person or by an advocate or an agent duly authorized on 13th day of July 2023 at 8:30 a.m. when this suit will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** that should you default to enter appearance in court on the day time mentioned above, the suit will proceed and judgement may be given in your absence.

Given under my hand and the seal of the court this 3rd day of July 2023

RESIDENT MAGISTRATE

---

## TANGAZO GARI LINAUZWA

Gari aina ya **TOYOTA HILUX** lenye namba za usajili **T164DXV** linauzwa lipo katika hali nzuri.

### Taarifa za Gari

Aina ya gari: **Toyota Hilux**
Mwaka wa kutengenezwa gari: **2004**
Mafuta inayotumia: **Diesel**
Model Namba: **KF-LN167**
Uwezo wa injini: **2980**
Aina ya bodi: **Station Wagon**
Rangi ya gari: **Multi Colour**
Chesesi namba: **LN1670032032**
Namba ya injini: **5L5506667**
Kilometa ilizotembea: **110197**




**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**Piga: 0757823350 / 0692793423**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha KIHONDA**
**Mkoa wa MOROGORO**
**JINAI Na. 204/2023**

**KUITWA SHAURINI MSHTAKIWA KATIKA SHAURI LA JINAI**
**(Aya ya 12 (1) ya nyongeza ya III ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu Sura ya 11)**

Mlalamikaji: **TABIA HASSAN**
Mshtakiwa: **CHRISTINA MKUMBO**
Kwa: **CHRISTINA MKUMBO wa MPANDA**

**K.K HAKIMU MKAZI MFAWIDHI, MAHAKAMA YA MWANZO/ WILAYA YA KIHONDA S.L.P 660 MOROGORO**

**UNAAMRIWA** uhudhurie mbele ya Mahakama hii **Tarehe 11 Mwezi 07 Mwaka 2023 Saa 03:00 Asubuhi** ukiwa ni mshtakiwa katika shauri lililotajwa hapo juu bila kukosa.

**Endapo** hautohudhuria katika siku iliyopangwa, hati ya kukukamata itatolewa.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo **Tarehe 30 Mwezi 06 Mwaka 2023**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA
MOROGORO

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**WILL MWANDASILA MAJUBA,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji yenye namba za usajili MC. 159 CKP, yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi ni **TDM/RB/2090/023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZHANG KAITONG** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALPHARD** yenye usajili namba: **T 595 ECC**, CHASSIS NAMBA: **ANH258003195** na ENGINE NAMBA: **2AZG550987.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **TAN/TAN/RB/176976/2023**

---


***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni IndustRial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mob: +255 - 0782253676***

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Alliance One yatoa vifaa vya TEHAMA kwa AMCOS

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

KAMPUNI ya Alliance One Tobacco Tanzania Limited (AOTTL) imeibuka mshindi wa pili kwa taasisi zisizo za kiserikali katika Siku ya Vyama vya Ushirika Duniani iliyoadhimishwa kitaifa mkoani Tabora.

Vilevile, kampuni hiyo imetoa msaada wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 30 kwa vyama vitano vya msingi vya tumbaku vinavyofanya vizuri zaidi, ukijumuisha kompyuta mpakato na fulana.

Kampuni hiyo iliibuka mshindi kupitia banda lake la maonesho ambalo wakulima wengi walitembelea kwa ajili ya kuelimishwa kuhusu masuala ya sekta ndogo ya tumbaku.

Tuzo hizo kwa kampuni hiyo na vyama vya msingi zilitolewa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, mwishoni mwa wiki.

Msemaji wa kampuni hiyo, Wakili John Magoti, alisema Alliance One imeshinda taji la mshindi wa pili si kwa bahati, bali kumetokana na kampuni kuzingatia kanuni za kilimo bora na kuwajali wakulima walioingia mkataba.

"Mchango wetu huu kwa wakulima unalenga kuboresha uwekaji kumbukumbu katika vyama vya msingi vya tumbaku kutoka kutumia karatasi za kawaida zinazochosha hadi kuhamia katika matumizi ya teknolojia ya kisasa ya habari na mawasiliano," alisema.

Vyama vitano vya ushirika wa masoko ya kilimo (AMCOS) vilivyopokea msaada ni Ibambala cha wilayani Kahama mkoani Shinyanga; Mgwezi cha mkoani Kigoma; Imalaupina cha wilayani Sikonge mkoani Tabora; Twendepamoja Kalunde cha mkoani Tabora; na Kombe cha wilayani Urambo mkoani Tabora.

Katika salamu zake za shukrani, Mwenyekiti wa AMCOS ya Ibambala, Faida Paul, alipongeza ukarimu wa Kampuni ya Alliance One Tobacco Tanzania Limited na kusema kuanzia sasa malalamiko yote yasiyo ya lazima kutoka kwa wanachama wake kuhusu uwekaji mbovu wa kumbukumbu yatakuwa historia.

"Matumizi ya kompyuta katika kutunza kumbukumbu za kilimo ni njia bora ya kutatua migogoro isiyo ya lazima miongoni mwa wanachama, hivyo tunaishukuru sana Alliance One kwa kuja kutuokoa," alipongeza.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa AMCOS ya Mgwezi yenye maskani yake mjini Kigoma, Gilbert Makwaya, alisema kupatiwa kompyuta za kusaidia uendeshaji na usimamiaji wa shughuli zao kumekuja wakati mwafaka.

"Serikali hivi karibuni imezindua mfumo wa taarifa kwa ajili ya kusimamia vyama vya ushirika, hivyo msaada huu kwetu wa vitu vinavyohitajika katika TEHAMA umekuja kwa wakati mwafaka," alisifu.

Mwanzoni mwa wiki iliyopita, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alitembelea banda la kampuni hiyo, akiipongeza kwa utendaji ubora katika sekta ndogo ya tumbaku.

Alitembezwa katika banda la kampuni hiyo na Mkurugenzi wa Kilimo wa kampuni hiyo, David Mayunga, aliyemweleza naibu waziri kuwa kampuni hiyo inawalipa wakulima kwa wakati kulingana na maagizo ya serikali.

"Kwetu hakuna malalamiko, tunalipa wakulima kwa wakati, ninamaanisha kila baada ya saa 48," alitamba.

# Wananchi wachangishana kujenga shule ya sekondari

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAKAZI wa mitaa sita ya Kata ya Mkuza, Halmashauri ya Mji wa Kibaha, wameridhia kuchanga fedha ili kununua eneo kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari.

Ujenzi huo wa shule una lengo la kuwaondolea kero watoto kutembea umbali wa kilometa nne mpaka tano kwenda Shule ya Sekondari Nyumbu.

Wamefikia makubaliano ya kila kaya kuchanga Sh. 20,000 wakiwa na lengo la kukusanya Sh. milioni 87.1 kununua eneo la kujenga shule yao ya sekondari kwa ajili ya watoto wanaotoka katika mitaa hiyo.

Makubaliano hayo ambayo yalifikiwa mwishoni mwa mwezi uliopita, yanatarajiwa kutekelezwa hadi ifikapo Julai 31, mwaka huu, tarehe ambayo kila kaya ikitakiwa iwe imekamilisha kutoa kiasi hicho (Sh. 20,000).

Katika maazimio hayo, pia walikubaliana kwa mwananchi mwenye uwezo lakini hachangii, hatopewa huduma katika ofisi za mitaa na kata ikiwamo ya kupitishiwa barua ya mikopo na utambulisho.

Ni makubaliano yaliyofikiwa wakati wananchi hao walipoitisha mkutano uliokuwa na ajenda ya kuona eneo husika na uhamasishaji wa upatikanaji wa fedha za ununuzi wa eneo lenye ekari 4.5 la ujenzi wa sekondari hiyo itakayoitwa Mbwate.

Katika mkutano huo, mmoja wa wakazi hao, George Kuguru, alisema uamuzi wa wananchi kuonyeshwa eneo husika umeleta faraja na ari ya watu wengi kuona umuhimu wa kuchangia fedha hizo tofauti na awali ambapo waliambiwa wachangie huku wakiwa hawajui eneo lilipo.

Nurdin Mambo, mkazi mwingine wa kata hiyo, alishauri michango hiyo iwaguse watu wenye viwanja na hawajajenga katika kata hiyo badala ya kuwalenga wanaoishi ndani ya kata hiyo pekee.

Awali Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Mbwate, Juma Msulwa, aliwaeleza wananchi hao kuwa michango hiyo ni mali ya halmashauri na ndio maana fedha zinawekwa katika akaunti ya maendeleo ya mtaa huo na wao kama mtaa ni wakusanyaji tu.

'Ikibainika una nguvu na hujalipa huu mchango, basi usije Ofisi ya Mtaa kutaka huduma maana hatukupi. Nenda popote pale, ninasisitiza usiende ofisini kama hujalipa huu mchango," alitoa angalizo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mbwate, Abdala Mtandio, aliomba mabalozi wa mitaa hiyo kukusanya michango hiyo kwa weledi ili kufanikisha lengo lao hilo.

Diwani wa Mkuza, Fokasi Bundala, alisema mchango huo ulipitishwa katika vikao mbalimbali vilivyofanyika mwishoni mwa mwaka 2022 ngazi ya tawi, mtaa na mkutano mkubwa ngazi ya kata uliofanyika Desemba 17, 2022.

Bundala alisema kuwa kupitia mikutano hiyo ilipitishwa kwamba wenye uwezo kifedha, wote wachangie kiasi hicho na asiyeshiriki hata kwa kidogo, basi hataki kushirikiana na serikali ya eneo hilo, hivyo nao hawatotoa ushirikiano kwake.

Kata ya Mkuza ina mitaa sita ya Bungo, Mkongoni, Kibondeni, Mpakani, Mbwate na Mkuza na ina kaya 924 zenye wakazi 2,364.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaelekeza katika Ibara yake ya 8(1)(d) kuwa: "Wananchi watashiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii."




Katibu wa CHADEMA Kanda ya Serengeti, Jackson Mnyawami (wa pili kulia), akimkabidhi mifuko mitano ya saruji katibu wa chama hicho Wilaya ya Musoma mkoani Mara, Donald Mwembe, juzi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya chama ya wilaya. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# Mali za mfungwa zataifishwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imeridhia mali za mfungwa Yanga Omari Yanga, vikiwamo viwanja saba, kutaifishwa, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 229.

Uamuzi huo wa mahakama ulifikiwa mwishoni mwa wiki baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini kuwasilisha maombi dhidi ya Yanga, yakisikilizwa na Jaji Elinaza Luvanda.

Mfungwa Omari Yanga alitiwa hatiani na kuhukumiwa kwenda jela miaka 30 mwaka 2020 kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin yenye uzito wa gramu 1052.63.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Sabrina Joshi huku upande wa utetezi ukiwakilishwa na Wakili Nehemia Mkoko.

Mahakama hiyo katika uamuzi wake ilikubaliana na maombi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwamba mali hizo ni mazalia ya uhalifu uliotokana na usafirishaji wa dawa za kulevya na sheria inaelekeza kuwa mali zote zinazopatikana kwa njia ya uhalifu ni lazima zitaifishwe ili kutoa fundisho kwa jamii kuwa uhalifu haulipi.

Mali zilizotaifishwa na mahakama ni: Kiwanja namba 32 Block 'C' Magaoni, Manispaa ya Tanga; kiwanja namba 73 Block 'A' Mwambani, Tanga; kiwanja namba 144 Block 'B' Mwakidila, Tanga; na kiwanja namba 615 na 617 Block 'B' cha Kange, Tanga.

Vingine ni: Kiwanja namba 30 Block 'C' Mwakidila/Magoani, Tanga, kiwanja namba 605 Block 'A' Mwambani, Tanga; na kiwanja namba 606 Block 'A' Mwambani, Tanga.

Mali hizo zote zipo mkoani Tanga na zina thamani ya Sh. milioni 229.

HABARI MICHEZO

# MTIBWA SUGAR U-20 YATOA SIRI KUZOA KILA KITU LIGI YA VIJANA

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

WAKATI timu ya vijana chini ya miaka 20 ya Mtibwa Sugar ikitwaa ubingwa wa Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu chini ya miaka hiyo, kocha wa kikosi hicho, Awadhi Juma ametoa siri ya mafanikio hayo.

Timu hiyo imetwaa ubingwa huo baada ya kuichapa timu ya Geita Gold FC bao 1-0 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi juzi kwa dakika 120.

Mbali na kutwaa ubingwa mara tano mfululizo, Mtibwa Sugar imezoa zawadi zote, Makambo akiwa mfungaji bora kwa mabao saba, kipa bora akiwa Toba Kutisha na mchezaji bora wa ligi hiyo ni kiungo mshambilijia wao, Ladaki Chambasi.

Mtibwa Sugar ilifika fainali baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Azam FC kwenye mechi ya nusu fainali huku Geita Gold FC ikiichapa Kagera Sugar mabao 2-0 katika hatua hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar U-20, Awadhi, alisema mafanikio hayo yametokana na maandalizi mazuri pamoja na mazoezi ya muda mrefu waliyoyafanya.

"Mafanikio haya yametokana na maandalizi ya muda mrefu ambayo tumekuwa tukiyafanya, vile vile umakini wa wachezaji wangu," alisema Juma.

Alisema ligi ya msimu huu ilikuwa na ushindani kwani kila timu ilijipanga vema kuhakikisha haipotezi mchezo wake hata mmoja.

Aidha, aliwataka wachezaji wake hao kutobweteke na ubingwa huo bali waongeze juhudi ya kufanya mazoezi ili wapate nafasi ya kuitwa kwenye timu kubwa.

Katika hatua nyingine mfungaji pekee wa bao hilo, Athumani Masumbuko 'Makambo', amesema ameiva kwa ajili ya kucheza Ligi Kuu, lakini bado kuna vitu anatakiwa aongeze ili aweze kuhimili ushindani.

Makambo alisema bao alilofunga pamoja na Kiatu cha Dhahabu alichotwaa, vyote hivyo vimemfanya kuzidi kujiamini na kujiona ni wakati sahihi wa kucheza Ligi Kuu japo anaamini bado kuna vitu anatakiwa kuongezewa na makocha wake kwani kuna ushindani mkubwa.

Akizungumzia kushangilia kupita kiasi baada ya kufunga bao pekee dakika ya 98, kutokana na kuongezwa dakika 30 baada ya kutopatikana mshindi kwa dakika 90 za mchezo, Makambo alisema kwanza kabisa ilikuwa ni kufikisha bao la saba ambalo lilimthibitishia kuwa angekuwa mfungaji bora kwa kumpita straika wa Azam FC, Cyprian Kichwele aliyemaliza mashindano na mabao sita.

"Wakati tunakuja uwanjani kwenye gari, naona mwenzangu tunayeshindana naye Kichwele ameshapiga 'hat-trick', tayari ana mabao sita, iliniuma sana hata kocha wangu, Awadhi Juma aliona nimenyong'onyea, akanituliza akaniambia kwanza tunapigania timu iwe bingwa siyo mimi kuwa mfungaji bora, kwa hiyo lile bao lilifanya mambo mawili kwa wakati mmoja, kunipa ufungaji bora na timu yangu kuwa bingwa," alisema Makambo.

Kichwele alifunga mabao yote matatu, Azam ikiifunga Kagera Sugar mabao 3-1, ikiwa ni mechi ya kusaka mshindi wa tatu kwenye uwanja huo, kabla ya fainali.



Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi nchini, Steven Mguto, akimkabidhi kombe nahodha wa Mtibwa Sugar U-20, Ladaki Chasambi, baada ya timu hiyo kutwaa ubingwa wa Ligi ya Vijana chini ya miaka 20, kwa kuifunga Geita Gold FC bao 1-0 , katika mechi ya fainali iliyopigwa juzi Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Jibril afunguka kilichomleta Azam FC

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji mpya wa Azam FC, Jibril Sillah, raia wa Gambia, amefunguka kwa mara ya kwanza tangu atue nchini kuwa kilichomleta kwenye klabu hiyo ni mipango endelevu na miundombinu aliyoiona, hivyo kuona ni sehemu sahihi kwake kuweza kuipa mafanikio na kutangaza jina lake ndani na nje ya mipaka ya bara la Afrika.

Kiungo huyo alitua nchini Jumapili na kwa mara ya kwanza alishuhudia mechi ya fainali ya vijana chini miaka 20 kati ya Mtibwa Sugar na Geita Gold kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam. "Nashukuru kila mmoja, mashabiki wa klabu hii, na watu wote waliofanikisha hili, nimekuja hapa kwa sababu namfahamu kocha Youssouph Dabo na najua kuwa klabu hii inakua, wakala wangu alinieleza vizuri kuhusu klabu hii, kwa hiyo nimekuja kuisaidia timu ili tuandike historia kwa pamoja, tushinde mataji pamoja na iendelee kukua," alisema mchezaji huyo.

Alisema haikuwa rahisi yeye kuja Tanzania kwa sababu alikuwa amepata ofa nyingi kutoka klabu mbalimbali Afrika.

"Nilikuwa nimepata ofa nyingi lakini nimeona mpango wa maendeleo ya klabu hii na mimi bado ni kijana, kwa mipango na miundombinu yake imenivutia mimi pamoja na kocha wangu, hivyo nikasema acha niende Azam naweza kuendelea zaidi pale na kuzidi kutangaza jina langu," alifichua mchezaji huyo sababu za kukubali kujiunga na klabu hiyo.

Mchezaji huyo anayekipiga pia kwenye Timu ya Taifa ya Gambia chini ya miaka 23, alikuwa akiichezea Klabu ya Jeunesse Sportive ya Morocco kwa mkopo kutoka Raja Athletic Club ya Casablanca ya nchini humo.

Ni mchezaji wa kwanza wa kigeni kusajiliwa msimu huu na Azam FC, huku uongozi ukibainisha kuwa utasajili wachezaji wengine wawili tu ili kufunga msimu.

"Awali tulidhani tunaweza kusajili wachezaji wasiopungua saba kwa ajili ya msimu ujao, lakini kwa yeye mwalimu Dabo alivyowaona wachezaji kwenye mechi za mwisho wa ligi, akatuambia hakuna haja ya kufanya usajili mkubwa, akataka wachezaji watatu tu wa kigeni ambao ni wapya kabisa na ukiongeza na mzawa ambaye ni Feisal Salum, kwa hiyo hapo ni kwamba sasa tumebakisha kuwatambulisha wachezaji wawili tu," alisema msemaji wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe.

Mbali na Ligi Kuu, Kombe la Mapinduzi, Ngao ya Jamii na FA, Azam itacheza michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika kwa msimu ujao.

## Pluijm kufungwa zaidi Singida FG

**Na Abdallah Mataka**

BAADA ya kuvutiwa na mafanikio waliyoyapata katika msimu wao wa kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara tangu ilipopanda kwa mara ya kwanza, uongozi wa Klabu ya Singida Fountain Gate, umesema upo katika mazungumzo na benchi lao la ufundi linaloongozwa na Kocha Hans van der Pluijm, ili kuendelea kukiokoa kikosi hicho.

Singida Fountain Gate, ambayo ilipanda Ligi Kuu msimu uliopita, imemaliza nafasi ya nne kwenye ligi hiyo na kukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho Afrika kwa msimu ujao.

Benchi hilo ambalo limeiongoza timu hiyo kufikia malengo ambayo waliwekewa kabla kuanza kwa msimu wa Ligi Kuu iliyomalizika, mkataba wa Van Pluijm unamalizika hivyo, klabu hiyo ipo kwenye mazungumzo ili kocha huyo raia wa Serbia aendelee kuinoa na wasaidizi wake.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa timu hiyo, Hussein Masanza, alisema benchi lao la ufundi limekuwa na msimu mzuri na limefanya kazi yake vizuri hivyo bado wanaimani nalo.

"Benchi letu la ufundi limetimiza malengo yetu kwa asilimia 100, tumemaliza nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ambayo yalikuwa malengo ya msimu uliomalizika, limetuvusha kushiriki michuano ya kimataifa.

"Hayo ni malengo makuu mawili limetimiza na ziada kwa ni kutufikisha fainali ya Kombe la Mapinduzi na nusu fainali Kombe la Shirikisho la Soka nchini (FA Cup), kwa hiyo umekuwa msimu mzuri sana kwa kocha na benchi zima la ufundi," alisema.

Masanza aliongeza kuwa Singida Fountain Gate FC bado ina mpango wa kuendelea na kocha huyo pamoja na benchi lake lote la ufundi.

"Mpaka sasa hakuna mabadiliko yoyote ambayo tumefanya katika benchi letu la ufundi na tunatarajia timu itaingia kambini Julai 6, mwaka huu ikiwa chini ya kocha Hans na benchi lake lote la ufundi," alisema.

Aidha, Masanza alisema kuwa awali timu hiyo ilikuwa iondoke moja kwa moja kuelekea Tunisia, lakini baada ya kikao cha bodi ya wakurugenzi ambacho kilikaa kwa mara ya kwanza wiki iliyopita, kimefikia makubaliano kwamba wachezaji wote ambao wamekwenda likizo na wale ambao wamesajiliwa wakutane kwanza ili wafahamiane wafanye mazoezi kwa pamoja kabla ya kuelekea Tunisia kwenye kambi ya wiki mbili.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE BEI JUU
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24, anataka kitita cha pauni milioni 206 ili kujiunga na klabu yoyote msimu huu wa majira ya joto. **(Mail)**

### GVARDIOL AKARIBIA CITY
MLINZI wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 21, anakaribia kujiunga Manchester City kwa mkataba wa pauni milioni 86. **(Telegraph)**

### SILVA AKATAA OFA SAUDIA
KOCHA wa Fulham, Marco Silva mwenye umri wa miaka 45, amekataa ofa ya mkataba wa pauni milioni 17 kutoka Ligi Kuu ya Soka Saudi Arabia. **(iNews)**

### LAPORTE AVUTIWA ARSENAL
MCHEZAJI Aymeric Laporte anavutiwa na Klabu za Arsenal na Juventus, huku mustakabali wa beki huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 29, katika Klabu ya Manchester City ukikumbwa na hali ya sintofahamu. **(Mundo Deportivo)**

### PULISIC AWANIWA MILAN
KLABU ya AC Milan imetoa ofa ya euro milioni 14 kumnunua winga wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic, 24. **(The Athletic)**

### WALKER KUUZWA BAYERN
KLABU ya Manchester City wanania ya kumuuza beki wa England, Kyle Walker mwenye umri wa miaka 33, ambaye amekuwa akiwindwa na Bayern Munich na wanatarajia kumpa mkataba mpya. **(Fabrizio Romano)**

### COLLINS SAFI BRENTFORD
KLABU ya Brentford imekubali ada ya pauni milioni 23 kutoka Wolves ya kumsajili beki wa Jamhuri ya Ireland, Nathan Collins, 22. **(Sky Sports)**


### KILMAN AWINDWA NAPOLI
MABINGWA wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Napoli wanahofia dau la euro milioni 35 litakataliwa na Wolves kwa ajili ya beki, Max Kilman, 26. **(The Athletics)**

### SOLOMON KUJIUNGA SPURS
MCHEZAJI wa zamani wa Fulham, Manor Solomon mwenye umri wa miaka 23, anatazamiwa kujiunga na Tottenham Hotspur. **(The Athletics)**

### LINGARD ANUKIA MIAMI
KIUNGO wa kati wa zamani wa Manchester United na Nottingham Forest, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 30, anafanya mazoezi na klabu ya soka ya Marekani, Inter Miami. **(Mirror)**

### BUFFON ATAKIWA SAUDIA
GOLIKIPA wa zamani wa Juventus, Paris St-Germain na Italia, Gianluigi Buffon mwenye umri wa miaka 45, amepewa ofa ya pauni milioni 25 kwa mwaka ili kuhamia Saudi Arabia. **(Mail)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI ATUMIA MIAKA MITATU KUKUBALI KUTUA INTER MIAMI

Mwaka 2019 wakati akiwa bado Barcelona, tulianza kufikiria jinsi ya kumleta, lakini...

**NEW YORK, Marekani**

MMILIKI wa Klabu ya Inter Miami CF, Jorge Mas, amesema ilimchukua miaka mitatu ya mazungumzo kumleta Lionel Messi katika klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Soka Marekani, MLS.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia 2022, akiwa na Argentina, Messi alitangaza mwezi uliopita kuwa atajiunga na Inter Miami kama mchezaji huru baada ya misimu miwili kule Paris Saint-Germain.

"Mwaka 2019 wakati Messi akiwa bado Barcelona, tulianza kufikiria jinsi ya kumleta," alisema Mas akiliambia gazeti la Hispania la El Pais.

"Nilitumia miaka mitatu kulishughulikia hili, mwaka mmoja na nusu nikifanya kazi kwa bidii sana. Kulikuwa na mazungumzo mengi na baba yake Messi ambaye ni wakala wake, Jorge.

"Mmiliki mwenzangu wa Inter Miami, David Beckham, alizungumza na Leo kuhusu masuala ya soka tu, kwa sababu alikuwa mchezaji."

Messi mwenye umri wa miaka 36, awali alikuwa amefikiria kurejea Barca, klabu ambayo aliiacha mwaka 2021 kutokana na matatizo yake ya kifedha, huku pia akikataa mkataba mnono kutoka Saudi Arabia.

"Niliona kama imefanywa mwishoni mwa Mei," Mas alisema. "Sikutaka ajisikie chini ya shinikizo. Tulikuwa tumezungumza kule Barcelona, Miami, Rosario, Doha ... nilitumia Kombe zima la Dunia kule Qatar, nikiitazama Argentina.


"Mkataba wa Apple ulikuwa muhimu sana kufunga mpango huo."

Messi, ambaye yuko likizo, anatarajiwa kusaini mkataba na Inter Miami hadi Desemba 2025, na chaguo la kuongeza mwaka mmoja, wakati Mas alithibitisha kuwa fowadi huyo atalipwa "kati ya pauni milioni 50 na 60 kwa mwaka."

Mas pia alithibitisha nia ya muda mrefu ya kumzunguka Messi na wachezaji anaowafahamu, wakiwamo Sergio Busquets na Jordi Alba. Pia alisema Miami itasajili wachezaji "wawili au watatu" zaidi lakini akapuuza ripoti kwamba marafiki wawili wa karibu wa Messi -- fowadi wa zamani wa Barca, Luis Suarez na winga wa Argentina, Angel Di Maria - wanaweza kuwasili msimu huu wa majira ya joto.

## HABARI MICHEZO

# VIEIRA APATA TIMU MPYA UFARANSA



**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Ligi Kuu Ufaransa 'Ligue 1' ya Strasbourg imemteua Patrick Vieira kuwa kocha wake mpya kwa mkataba wa miaka mitatu, klabu na kumtangaza rasmi jana.

Mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa Ufaransa aliifundisha klabu ya Ligi Kuu ya England, Crystal Palace kuanzia 2021 hadi mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 47, aliiongoza Palace kumaliza katika nafasi ya 12 na nusu fainali ya Kombe la FA katika msimu wake wa kwanza akiwa kocha, lakini alitimuliwa katikati ya Machi baada ya kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Brighton & Hove Albion.

"Kuwasili kwa Patrick kunapaswa kuturuhusu kufanya maendeleo zaidi na kupiga hatua," alisema rais wa Strasbourg, Marc Keller.

"Analingana na wasifu tuliokuwa tunatafuta, kocha mwenye uzoefu wa kimataifa, na ambaye ana ufahamu mzuri wa Ligue 1 na wachezaji wake wachanga."

Vieira alishinda Kombe la Dunia mwaka 1998 na Ubingwa wa Ulaya mwaka 2000 kama mchezaji wa Ufaransa. Aliichezea nchi yake zaidi ya mechi 100, akifunga mabao sita.

Katika ngazi ya klabu, aliisaidia Arsenal kushinda mataji matatu ya Ligi Kuu England na kushinda Serie A mara nne akiwa na AC Milan mwaka 1995 hadi 1996 na akiwa na Inter Milan katika misimu mitatu mfululizo kuanzia 2006-07.

Mfaransa huyo alianza maisha yake ya ukocha akiwa na timu yake ya zamani ya Manchester City chini ya umri wa miaka 23 kuanzia mwaka 2013 hadi 2015, kabla ya kuchukua mikoba ya New York City FC na kisha Klabu ya Nice ya Ligue 1.

"Nina furaha hasa kujiunga na Racing," alisema Vieira akiiambia tovuti ya klabu. "Ninajua historia na utambulisho wa klabu hii."

Strasbourg ilimaliza katika nafasi ya 15 katika msimu wa ligi wa 2022-23.

# Man United yawania kumsajili Tchouameni




**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inajaribu kulipita dau la Arsenal la pauni milioni 85 kumnunua mshambuliaji wa Real Madrid, Aurelien Tchouameni.

Lakini Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, amemwongeza Tchouameni kwenye orodha yake fupi ya wachezaji anaowawania.

Kiungo huyo alipata shida kuwa kwenye kikosi cha kwanza katika Klabu ya Real Madrid msimu uliopita na inaaminika kuwa anaweza kupatikana kwa bei ndogo.

Kwa mujibu wa Nacional, United imeingia kwenye vita ya kutaka kumsajili mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa, kwani pia anawaniwa na klabu kadhaa za Ulaya.

Ripoti hiyo hiyo inadai kuwa bosi wa 'Mashetani Wekundu' hao, Erik ten Hag, "anaishinikiza" klabu hiyo kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

## Liverpool yamnasa rasmi Szoboszlai

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL imemsajili kiungo, Dominik Szoboszlai, kutoka Klabu ya RB Leipzig ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, miamba hiyo ya Ligi Kuu England imetangaza.

Nahodha huyo wa Hungary anawasili Anfield baada ya vyanzo vya habari kuiambia ESPN kuwa klabu hiyo imetimiza kipengele chake cha kumnunua cha euro milioni 70 kutoka katika mkataba wake.

Szoboszlai mwenye umri wa miaka 22, anakuwa mchezaji wa pili kusajiliwa na klabu hiyo chini ya Mkurugenzi mpya wa Michezo, Jorg Schmadtke, baada ya Alexis Mac Allister, huku Liverpool wakitarajia kurekebisha safu yao ya kiungo kutokana na msimu mbaya.

"Siku tatu au nne zilizopita haikuwa rahisi. Lakini mwisho niko hapa, nina furaha na nasubiri kwa hamu kubwa kuichezea klabu hii.

"Klabu ya kihistoria, wachezaji wazuri sana, kocha mzuri, kila kitu ni kizuri. Kwangu ilikuwa sawa kupiga hatua inayofuata katika klabu kama hii. Mashabiki, uwanja, kila kitu ni kizuri."

Raia huyo wa Hungary alifunga mabao 20 na kutoa asisti 22 katika michezo 91 tangu ajiunge na Leipzig katika dirisha la usajili la msimu wa baridi wa 2021.

Szoboszlai aliisaidia Leipzig kushinda tena mataji ya Ujerumani na alifunga bao lao la pili walipoilaza Eintracht Frankfurt 2-0 katika fainali ya msimu uliopita mapema Juni.



HABARI MICHEZO

# SPORTPESA YAIJAZA MAMILIONI YA BONASI SINGIDA FOUNTAIN GATE FC

**Na Shufaa Lyimo**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubashiri nchini ya SportPesa, imeikabidhi timu ya Singida Fountain Gate, kitita cha Sh. milioni 50 ikiwa ni bonasi ya kumaliza nafasi ya nne katika msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana wakati wa makabidhiano hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa Tanzania, Abbas Tarimba, alisema wametoa fedha hizo kama motisha kutokana na kuridhishwa na juhudi zilizofanywa na timu hiyo.

"Tumetoa fedha hizi kama motisha kwa ajili ya kuridhishwa na juhudi iliyofanywa na timu hii msimu uliopita, endapo wangemaliza wakiwa juu tungewapa kubwa zaidi ya hii tuliyowapa leo," alisema Tarimba.

Mkurugenzi huyo alisema timu hiyo imepiga hatua kubwa kwenye Ligi Kuu jambo ambalo linazidi kuwapa matumaini ya kuendelea kufanya nao kazi huku akiwapongeza kwa kufanikiwa kupata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao.

"Nachukua pia fursa hii, kuwapongeza kwa kufanikiwa kupata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa, ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, msimu unaoanzia 2023/2024," alisema.

Kwa upande wa Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Singida Fountain Gate, John Kadutu, amejigamba kuwa fedha hizo zimewaongezea hamasa na kuwataka waliopo juu yao wajipange msimu ujao kutokana na aina ya usajili wanaokwenda kuufanya.

"Tutahakikisha msimu ujao tunazishusha timu zilizopo juu kutokana na usajili tutakaoufanya," alisema Kidutu.

Alisema mafanikio hayo yametokana na udhamini huo na kuahidi kuongeza ushindani tofauti na walioufanya msimu huo.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 50, Makamu wa Rais wa Singida Fountain Gate FC, John Kadutu, ikiwa ni bonasi ya kumaliza nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu Bara. Wanaoshuhudia katikati ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya na wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa Masoko Singida FC, Tabitha Kidawawa. **MPIGAPICHA WETU**

# Mkude atabiriwa makubwa Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema iwapo kiungo wake wa zamani Jonas Mkude atatua Klabu ya Yanga, watakuwa wamelamba dume na kuwa wa thamani kubwa kwani atakuwa ndiye mchezaji pekee ambaye amewahi kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwenye kikosi hicho.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alisema amesikia taarifa za mchezaji huyo kuwaniwa na watani zao wa jadi, Yanga, na kusema iwapo atatua kwenye kikosi hicho cha Wanajangwani atakuwa mchezaji wa kiwango cha juu sana kuliko aliowakuta.

"Kama atakwenda huko anakokwenda atakuwa mchezaji wa kiwango cha juu, na atakuwa mchezaji mwenye wasifu mkubwa zaidi, kwa sababu atakutana na wachezaji ambao hawajawahi kucheza hata hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa, kwa hiyo kwao atakuwa ni mchezaji mwenye thamani kubwa, kusema kweli wamelamba dume kwao wao, atawasaidia kwa sehemu kubwa sana na sisi Simba roho yetu ni nyeupe kabisa," alisema Ahmed.

Akizungumzia sababu za kuondoka Simba, Ahmed alisema kuwa si kwa sababu kiwango chake kimeshuka, ila ni za kiufundi zaidi.

"Mkude kama Simba tungemhitaji angebaki, asingeweza kukataa kubaki, ameishi Simba ngumu kweli kweli, usajili wa kuchangishana, wakati huo Yanga na Azam zote mbili zikiwa na uwezo mkubwa na walikuwa wanamhitaji, lakini alibaki, hivyo kulikuwa hakuna namna yoyote kuondoka yeye kipindi hiki cha neema na maisha bora, ameondoka kwa sababu za kiufundi.

"Tungependa kuendelea kubaki naye, lakini kwa sasa tunataka kuifanya timu iwe ya kiushindani zaidi, watu wanahitaji matokeo mazuri leo na kesho, kwa hiyo huwezi kubaki na mtu ambaye unaona kiufundi hatoweza kuwasaidia, ila anakokwenda atakuwa supa staa," alisisitiza.

Alikanusha taarifa zinazosambazwa kuwa Simba ilishindwana naye dau hivyo kutimkia Yanga, akisema hizo zimekuwa ni tabia ya wenzao wa upande wa pili.

"Kwanza wanachokifanya upande wa pili wanatengeneza mazingira ionekane wametunyang'anya au wametupiga bao, ukweli utabaki pale pale kuwa watakuwa wamemchukua mchezaji ambaye Simba tumemuacha, na huo umekuwa ndiyo utamaduni wao kwa miaka yote, tulimuacha Bernard Morrison wakamchukua, tumemuacha Mkude naye nasikia wamemchukua, kwa hiyo wao levo yao ndiyo hiyo," alibainisha Meneja Habari huyo.

# Yanga, Big Bullets kuvaana Malawi

INATOKA UK. 24

zao bado hazijamalizika.

"Ukisikia Yanga wanamfukuzia mchezaji fulani ujue si kweli, tayari tumeshasajili wachezaji wote tuliokuwa tunawahitaji wa ndani na nje, kilichobaki ni kuwatangaza tu, na wale ambao hatutokuwa nao msimu ujao bado tutaendelea kuwapa 'thank you' zao, bado hazijaisha," alisema.

Alibainisha kuwa msimu mpya wa Yanga utaaanza Julai 10, mwaka huu ambapo wachezaji wote wa zamani na wapya wataanza kuripoti na baada ya hapo ndipo wataambiwa kama kambi itakuwa hapa nchini au la.

"Wataanza kuwasili mmoja mmoja kuanzia Julai 10, na kikosi kikikamilika sasa hapo wataambiwa kama kambi itakuwa pale pale tulipo siku zote, tutatoka nje ya nchi au vinginevyo," alibainisha.


# Simba SC kambi sasa kumekucha

INATOKA UK. 24

mapumzikoni baada ya mashindano yote ya msimu kuanza," alisema Dk. Kagabo.

Simba imekuwa klabu ya kwanza kukusanya wachezaji wake na kuanza kuwapima afya kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa mashindano.

Klabu ya Azam kupitia kwa msemaji wake, Hasheem Ibwe, ilitangaza kuwa wachezaji wake wataanza kuwasili leo Jumanne kwa ajili ya zoezi kama hilo, kabla ya kuanza mazoezi na Julai 9 wanatarajia kuondoka nchini kwenda Tunisia kwa ajili ya 'preseason', kabla ya kurejea Julai 30, mwaka huu huku Yanga, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, akitanabaisha kuwa wachezaji wa timu hiyo wataanza kuingia kesho Julai 5 kwa ajili ya safari ya kwenda nchini Malawi, kwa mwaliko maalum wa serikali ya nchi hiyo wa maadhimisho ya Uhuru wa nchi hiyo Alhamisi wiki hii.



# Michezo

Jumanne Julai 4, 2023

Nipashe



**Messi atumia miaka mitatu kukubali kutua Inter Miami** UKURASA 21

# YANGA, BIG BULLETS KUVAANA MALAWI

**●●● Serikali nchini humo yawaalika, mastaa waitwa haraka, yatangaza kukamilisha usajili huku…**

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imealikwa nchini Malawi kwenye maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa nchi hiyo, ambapo inatarajiwa kucheza dhidi ya Nyasa Big Bullets siku ya kilele Alhamisi wiki hii.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa wamepokea mwaliko huo kutoka Serikali ya Malawi chini ya Rais Lazarus Chakwera, hivyo kwa heshima kubwa, pamoja na kwamba wachezaji wao wapo kwenye mapumziko baada ya kumalizika kwa msimu wa mashindano, wamewapigia simu warejee kwa ajili ya ziara hiyo.

"Tumepokea mwaliko maalum kutoka kwa Serikali ya Malawi kucheza mchezo maalum kwenye maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa Malawi, yatakayofanyika Julai 6, mwaka huu, ni heshima kubwa sana kwa nchi yetu na kwa taifa kwa ujumla.

"Hii ratiba haikuwapo awali, lakini kwa heshima waliotupa, uongozi ukapiga simu kwa wachezaji kuwataka kurejea, Julai 5, tunawashukuru wote walioitika wito huu, hivyo tutaondoka na kikosi cha kwanza cha wachezaji 15 na tutawaongeza na wa chini ya miaka 20, ambao watakuwa wachezaji wapato 21," alisema Kamwe.

Alisema umekuwa ni mwaliko wa kipekee na kihistoria, kwani watakuwa huko pamoja na Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suhulu Hassan, ambaye naye ni mmoja wa wageni wa heshima walioalikwa kwenye maadhimisho ya uhuru wa nchi hiyo uliopatikana mwaka 1964.

"Sisi Yanga tutawahi, halafu tutampokea rais wetu ambaye naye ni mmoja wa wageni wa heshima kwenye maadhimisho hayo atakapowasili nchini humo," alisema.

Alisema sherehe zitafanyika asubuhi mpaka mchana na jioni Yanga itajitupa kwenye Uwanja wa Bingu Mutharika kucheza dhidi ya Nyasa Big Bullets mabingwa wa msimu uliopita, lakini kwa sasa wakishika nafasi ya pili kwa pointi 22 ikicheza michezo 11, chini ya Silver Strikers yenye michezo kama hiyo na pointi 25.

Wakati hayo yakijiri, klabu hiyo imesema tayari imeshamaliza kufanya usajili wa wachezaji wa ndani na nje ya nchi na inachosubiri ni kuwatambulisha, huku ikisisitiza kuwa 'thank you'

INAENDELEA UK. 23



# MKUDE

## Atabiriwa makubwa akitua Yanga

UKURASA. 23

# Simba SC kambi sasa kumekucha

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeanza maandalizi ya msimu ujao wa mashindano kwa wachezaji wake kurejea kutoka mapumzikoni na kuanza vipimo vya afya kabla ya kuingia kambini rasmi mapema mwezi huu.

Jumla ya wachezaji 12 wa klabu hiyo wamefanyiwa vipimo jana kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dar es Salaam, kuangalia afya zao, kabla ya msimu mpya wa mashindano 2023/24 kuanza.

Daktari wa klabu hiyo, Edwin Kagabo, amesema zoezi limekwenda vizuri na hali za wachezaji ziko vema, ambapo amebainisha wamepimwa vipimo vyote vya msimu ambavyo mchezaji anapaswa kuangaliwa.

"Tumewapima wachezaji wetu vitu muhimu vinavyohitajika kwa mchezaji kama uzito wa mwili, wingi wa damu, ufanyaji kazi wa figo na ini, mionzi (X-ray), ufanyaji kazi wa umeme kwenye moyo ili tufahamu utimamu wao kabla ya kuanza msimu," alisema Dk. Kagabo.

Alisema zoezi hili litaendelea tena leo kwa kundi la pili kufanyiwa vipimo na kila kitu kikikamilika, basi ni ishara ya kuwashwa taa ya kijani kuelekea maandalizi ya msimu mpya wa ligi.

Miongoni mwa wachezaji waliofanyiwa vipimo jana ni Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', Mzamiru Yassin, Shomari Kapombe, Israel Patrick Mwenda na Kibu Denis.

Asilimia kubwa ya wachezaji walioimwa afya jana na watakaopimwa leo ni wale wazamani huku wachezaji wapya waliosajiliwa wakitarajiwa kufanyiwa vipimo punde tu baada ya kuwasili.

"Huu ni utaratibu wetu kabla ya kuanza maandalizi ya msimu, lazima tuwafanyie vipimo wachezaji ili kujua hali za afya zao wanapotoka

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >